# BUNGA LA TANZANIA

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kumi – Tarehe 12 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, karibuni katika juma la mwisho la Mkutano wa Tisa. Swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 129

### Barabara ya Kuunganisha Wilaya ya Sikonge na Urambo

**MHE. SAIDI J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara itakayo Tutuo – Mole-Usanganya –Izimbili hadi Urambo ndiyo barabara fupi ya kuunganisha Wilaya ya Sikonge na Urambo na kwa kuwa fedha zilizotengwa kwa barabara hiyo mara nyingi hazitoshelezi matengenezo yanayohitajika ili barabara hiyo iweze kupitika kwa majira yote:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongezea Fedha barabara hiyo ili iweze kupata matengenezo ya kuiimarisha zaidi?

(b) Je, Daraja lililopo Kitongoji cha Ibomba, ambalo limeharibika sana kutokana na mvua za msimu uliopita, litatengewa fedha za kutosha ili kujenga daraja linaloweza kuhimili maji mengi ya Mto huo hasa nyakati za mvua nyingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saida Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Tutuo-Mole-Usanganya-Izimbili hadi Urambo inayounganisha Wilaya ya Urambo Sikonge ina jumla ya urefu wa Km.71, kati ya hizi km 27 ziko upande wa Sikonge na km 44 ziko upande wa Urambo. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilitenga shilingi milioni 14.7 kwa matengenezo ya sehemu korofi ya barabara hiyo upande wa Sikonge.

Pia kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya Sikonge imetenga kiasi cha shilingi milioni 13.94 kwa matengenezo ya kawaida ya km 20 na shilingi milio ni 3.45 kwa matengenezo ya sehemu korofi wa km 3.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Halmashauri ya Urambo, imetenga kiasi cha shilingi milioni 29.27 kwa matengenezo ya kawaida urefu wa km 44 na kiasi cha shilingi milioni 49 kwa matengenezo ya muda maalum urefu wa km 7 kwa barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja la Ibomba, daraja lililopo ni zima isipokuwa uwezo wake wa kupitisha maji wakati wa mvua ndio hautoshelezi. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kwa kutumia fedha kutoka Mradi wa Usafiri katika Halmashauri itatumia kiasi cha shilingi milioni 31.35 kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa ajili ya uwekaji wa Makalvati Mistari minne ili kuongeza uwezo wa daraja kupitisha maji na kuweka changarawe sehemu ya juu ya daraja. Kama matengenezo hayo yatakamilika barabara hiyo itakuwa inapitika kwa wakati wote wa mwaka mzima.

**MHE. SAIDI J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii inatumiwa na viongozi wengi ukiwemo wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na baadhi ya viongozi, wajumbe wengi wa Kamati mbalimbali wameitumia barabara hii kutoka Sikonge kwenda Urambo au kwenda Urambo kuja Sikonge na kwa kuwa barabara hii inatuunganisha vile vile na Mikoa ya Magharibi na Kusini.

(a) Je, Serikali kwa nini isikubali barabara hii ikaipa hadhi ambayo inaweza ikastahili ili iweze kuhudumiwa na Mkoa kwa maana ya *TANROADS*?

(b) Kwa kuwa matengenezo ya daraja anayoyaeleza kwanza daraja lenyewe liko katika Wilaya ya Sikonge na maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ndiyo imetenga fedha. Sijui kama kitu cha namna hiyo kinaweza kikatokea. Lakini napenda anithibitishie kwamba kwa mwaka huu wa fedha daraja hilo limetengewa kiasi gani cha fedha ili kuhakikisha kwamba linapitika katika kipindi chote cha masika kwa sababu sasa hivi hali ni mbaya sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunafahamu kwamba barabara hiyo, ni kiungo muhimu sana kati ya Wilaya hizo mbili, pia kati ya Mkoa wa Tabora pamoja na Mikoa mingine ya Kaskazini. Kwa umuhimu wa barabara hii, mimi naomba tungojee sheria ambayo imepitishwa sheria ya barabara ambayo tumeipitisha hivi karibuni tuone uwezekano kwamba barabara hii imejumuishwa kuhudumiwa na Mkoa au ibaki Halmashauri. Tatizo, ambalo mimi naliona ni utengenezaji, aidha, limetengenezwa na Halmashauri au na *TANROAD*.

Kikubwa ambacho sisi tunasisitiza kwamba barabara hii itengenezwe ili kuimarisha uchumi wa sehemu hiyo na ili barabara hii iwe muhimu. Kwa hiyo, hilo Mheshimiwa Mbunge, tunalizingatia na tutaangalia pia uwezekano wa kuongeza fedha zaidi ili barabara hii iweze kupitika kwa mwaka mzima.

La pili, kuhusu matengenezo ya daraja la Ibomba nasisitiza kwamba fedha zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha hilo daraja na kwa mwaka huu fedha hizi zipo na zimekwishapelekwa na tumemwomba Mkurugenzi atangaze haraka ili daraja hili liweze kutengezwa kabla masika haijaanza. (*Makofi*)

Na. 130

**Mchakato wa Kuugawa Mkoa wa Mtwara**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa, yapo mapendekezo ya kuugawa Mkoa wa Mtwara kutokana na hali ya kijiografia, kijamii, wingi wa watu na lengo la kuweka mawasiliano bora zaidi kwa jamii ambazo ziko mbali kimipaka:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa kuanzisha mkoa mpya wa Kusini, ili Wilaya zilizoko karibu hasa Tunduru ambayo kwa muda mrefu imewekwa katika Mkoa wa Ruvuma na kusababisha kukosekana kwa mawasiliano mazuri ya barabara na simu?

(b) Je, ni Wilaya ngapi zitakazohusika na mchakato huo ambao wananchi wanaungojea kwa hamu?

(c) Je, ni lini Mji Mdogo wa Masasi utapandishwa hadhi ili uwe mji kamili na kusaidia kukua kwa miji mingine kama Ndanda, Mangaka, Chiungutwa na ksdhalika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Uanzishaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Katiba, pamoja na Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 kwa Mamlaka za Wilaya na sheria Na.8 kwa Mamlaka za Miji za mwaka 1982 na sheria ya taratibu za uanzishaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Ofisi yangu imekuwa ikipokea hoja mbalimbali kwa njia ya barua kutoka kwa wananchi na mijadala na maswali ya Wabunge kuhusu kuongeza mikoa mingine kwa kuunganisha baadhi ya Wilaya na kuanzisha Mikoa mipya kwa lengo la kupunguza ukubwa wa baadhi ya Mikoa.

(a) Mheshimiwa Spika, mchakato unaoendelea katika kuanzisha Mkoa mpya wa Kusini upo bado katika hatua ya awali kabisa ya kukusanya maoni ya wadau wenywe wa Mikoa husika. Ofisi yangu imeielekeza Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, kufanya kikao cha pamoja yaani *Inter Regional Meeting*, ili kuweza kuona kama kuna uwezekano wa kuunganisha baadhi ya Wilaya za Mikoa ili kuunda Mkoa mpya wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mikoa hiyo bado inaendelea na mchakato wa kufanya kikao hicho namshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mikoa hiyo, wavute subira hadi mchakato huu utakapokamilika.

(b) Kwa kuwa Mchakato huu haujakamilika kama nilivyoeleza kwenye majibu ya sehemu (a) Wilaya zitakazohusika hazijaweza kufahamika. Aidha kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuwahimiza viongozi wa Mikoa husika kukutana haraka ili kukamilisha zoezi hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaofuatwa ili eneo la utawala kama mji mdogo wa Masasi kupandishwa hadhi ya kuwa Mji umeelezwa na kufafanuliwa kwenye vifungu vya 20 na 21 vya sheria ya Serikali za Mitaa kwa Mamlaka za Wilaya Namba 7 ya mwaka 1982 na kifungu cha 5 cha Sheria ya Serikali za Mitaa kwa Mamlaka za Miji Namba 8 ya mwaka 1982.

Kwa mujibu wa Sheria hizi, uamuzi na utekelezaji wa mahitaji haya hufanywa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri husika na kuwasilisha ombi rasmi kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kupitia Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa.

Pia viko vigezo vinavyoainishwa katika sera ya taifa ya Maendeleo ya makazi ya mwaka 2000 ili mji mdogo au eneo lolote liweze kupewa hadhi ya mji. Vigezo hivyo ni pamoja na:-(i)Kuwa na idadi ya watu wasiopungua 30,000.(ii) Mji uwe na uwezo wa kujiendesha angalau kwa asilimia 50 ya Bajeti yake.(iii)Mji uwe na kiwango cha juu cha utoaji wa huduma za hospitali; kuwe na sekondari; kuwa na angalau maduka 50; kituo cha polisi; na eneo liwe makao makuu ya tarafa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, hajapokea ombi rasmi la kuanzishwa Halmashauri ya Mji wa Masasi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri na mimi nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Halmashauri ya Masasi imepitia vigezo mbalimbali kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kweli tuko mbali kabisa katika kukidhi vigezo hivi. Je, Waziri yuko tayari kukubali kwamba kama vigezo hivi tutavikamilisha mapema mamlaka ya Mji wa Masasi inaweza kuanzishwa mwezi Julai mwakani?

(b) Kwa kuwa katika Jimbo la Masasi, kuna kata ambazo ni kubwa sana ambazo hata Waziri anazifahamu. Je, katika kata ya Lukuledi ambayo ina vijiji zaidi ya 18 kata ya Lisekese ambayo ina vijiji zaidi ya 25. Je, kuna uwezekano upi wa kuanzisha kata mpya ili tuweze kuwahudumia vizuri zaidi wananchi wetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashauri ya Mji Mdogo wa Masasi imekidhi baadhi ya vigezo ambavyo ni pamoja na idadi ya watu kwa sasa hivi ina idadi ya watu 73,000 lakini kigezo cha uwezo wa kujiendesha angalau kwa asilimia 50 kigezo hiki hakijafikiwa. Lakini nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaomba maombi hayo yawasilishwe rasmi na yapitie kwenye vikao husika yaje ofisini kwetu ili na sisi tuyafanyie kazi tuone kwamba kuna uwezekano wa kupandisha hadhi Mji Mdogo wa Masasi ili kuwa Halmashauri ya Mji. Kuhusu suala la pili la ugawaji wa kata ni kweli nilifika Wilayani Masasi nilitembelea hizo kata za Lukuledi na Lisekese ni kata kubwa lakini kwa sasa tunafanya zoezi la ugawaji wa vijiji pamoja na tarafa. Kuhusu kata bado zoezi hili halijakamilika. Litakapokamilika Mheshimiwa Mbunge, maombi yake yatazingatiwa kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ombi la Mkoa wa Mtwara kupata Mkoa mpya linatokana na kukosa taarifa zinazotakiwa. Lakini ombi kama hilo limetolewa kwa Mkoa wa Iringa tukaambiwa tuhamishe Wilaya mojawapo. Waziri ambaye anajibu swali hivi sasa alishindwa kutembelea Wilaya za Ludewa na Makete alipotumwa na Waziri Mkuu kuangalia shule kwa sababu ya ugumu wa Jiografia, ubaya wa udongo na sababu nyingine. Je, uamuzi kutokugawa Mkoa wa Iringa ili wapate Mkoa wa Njombe unatokana na kukosa taarifa au vipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mzee Makwetta na Mzee Galinoma, nafikiri alikuwepo na Mbunge mwingine walikuja Ofisini tumezungumza juu ya ombi lao na kimsingi tuliseme tumelipokea tutalifanyia kazi na majibu tumesharejesha kwa Mkuu wa Mkoa. Kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Makwetta pamoja na Wabunge wengine. Kwa kuwa jambo hili sasa liko kwetu rasmi basi watupe nafasi tuweze kulifanyia uchambuzi wa kina tuone ni majibu gani tunaweza tukawapa.

Lakini niongeze tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maelekezo na nafikiri Mzee Makwetta anajua kwamba kwa maana ya kuanzisha Wilaya ya Njombe kwa sasa kuwa Mkoa ni jambo lisilowezekana. Lakini kwa kuunganisha Wilaya nyingine mbili ni jambo linaweza kufikiriwa na likatolewa uamuzi. Kwa hiyo, nafikiri tutafika mahali tutaelewana na wenzetu wa Mkoa wa Iringa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maelekezo ya Halmshauri nyingi huwa hazipendi kuitisha mikutano kwa ajili ya kupitia Halmashauri, kuwa na Halmashauri zingine ndogo na kuwa Halmashauri za Miji. Na kwa kuwa Serikali ilitoa waraka wa kupandisha miji ambayo ilikuwa Makao Makuu ya Wilaya zote nchini kuwa Halmashauri za Miji Midogo. Je, Serikali haiwezi ikatoa waraka vile vile kwa Halmashauri ambazo ni Makao Makuu za Wilaya kama Masasi, Nzega kuwa Halmashauri Kuu za Miji kamili hasa katika uchaguzi ujao wa 2009 ikaingia kama Halmashauri Kuu kamili kuliko kungoja Halmashauri zikae kwa sababu wakurugenzi huwa hawapendi kupatia ruhusu Halmashauri zipate Halmashauri zingine badala ya Halmashauri za Wilaya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye Bunge lililopita kwamba Mamlaka ya Miji Midogo 90 zilikwishatangazwa na tuliwaagiza Wakurugenzi wote waweze kutekeleza kuanzisha mamlaka za Miji Midogo. Kwa sasa hivi kama Serikali tumetoa tena agizo mpaka ifikapo tarehe 31 Desemba mwaka huu 2007 Halmashauri zote zihakikishe kwamba mamlaka za Miji Midogo ile 90 iliyotangazwa imetangazwa zimeanzishwa rasmi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Selelii, katika Halmashauri wahakikishe kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo imeanzishwa mara moja kabla ya tarehe 31 Desemba, 2007. *(Makofi)*

Na. 131

**Maji ya Ziwa Nyasa**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH (MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ziwa Nyasa lina majina mawili (Ziwa Nyasa na Ziwa Malawi); na kwa kuwa ziwa hilo ni chanzo kikubwa cha maji kwa matumizi ya binadamu (*domestic use*) na kilimo cha umwagiliaji *(Large Scale Irrigation Scheme):-*

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kunadi jina la Ziwa Nyasa ili kuondoa utata wa Malawi inayodai kuwa Ziwa hilo lote liko ndani ya nchi yao (*Territorial Rights)*

(b) Je, ni mikakati gani ya muda mrefu na muda mfupi ya kutumia maji ya Ziwa Nyasa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Ziwa Nyasa ni chanzo kikubwa cha maji kwa matumizi ya binadamu wanaolizunguka Ziwa na kwa kilimo cha umwagiliaji. Aidha, nakiri kuwa Ziwa hilo hujulikana kwa mjina tofauti katika nchi zinazolizunguka.

Kwa upande wa Tanzania Ziwa hilo linajulikana kwa jina la Ziwa Nyasa, kwa upande wa Malawi linaitwa Ziwa Malawi na kwa upande wa Msumbiji ni Ziwa Niasaa. Ziwa hilo lenye urefu wa kilomita 590 na upana kati ya kilomita 30 mpaka 80, lina ukubwa wa kilomita za mraba 33,457. Eneo la Tanzania ni kilomita za mraba 8,105 au asilimia 24.2, eneo la Malawi ni kilomita za mraba 19,372 (au 57.9%) wakati Msumbiji inamiliki eneo lenye kilomita za mraba 5,980 (au 17.9%).

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mahusiano mazuri na Malawi kwa muda mrefu sasa na wala haina mgogoro kuhusu jina la Ziwa Nyasa. Aidha, ni ukweli usiopingika kwamba sheria za wakati wa kikoloni ndiyo chimbuko la suala la Ziwa Nyasa.

Mkataba wa *Anglo German* ulibainisha kwamba Ziwa Nyasa ni milki ya Serikali ya Malawi kinyume na taratibu za sasa za mipaka inayopita majini, inayotoa fursa sawa kwa nchi zinazotenganishwa kwa Ziwa au Bahari, kwamba mpaka upitie katikati ya Ziwa au Bahari husika. Tanzania na Malawi zinaendelea kutumia Ziwa hilo kwa shughuli za kila siku bila ya mgogoro wa aina yoyote. Na pia zinaendelea kubuni miradi ya pamoja ya kuendeleza Bonde la Ziwa Nyasa.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika mpango kabambe wa Taifa wa kilimo cha Umwagiliaji ilibaini kwamba eneo linalofaa kwa umwagiliaji katika ukanda wa Ziwa Nyasa hususan Mkoa wa Ruvuma ni hekta 23,200 ambao uwezekano ni mkubwa, hekta 283,700 uwekezano wa kati na hekta 1,617,800 ni uwezekano wa kiwango cha chini. Baada ya kubaini uwezekano huu, Wizara imepanga kuanzisha ukanda wa Kijani wa Ziwa Nyasa (*Lake Nyasa Green Belt*) ambapo teknolojia rahisi za umwagiliaji zitatumika.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika nchi yetu ina matatizo ya maji mahali kwingi sana, maji ya kutumia na maji kwa ajili ya umwagiliaji ili kuendeleza kilimo. Matatizo haya yapo Iramba na naamini hata Urambo yapo na hata Monduli yapo matatizo haya. Kutokana na hali hiyo, lakini tumebahatika kuwa na mabwawa na maziwa mengi sana nchini.

(a) Je, Wizara ina mikakati gani ya kuhakikisha yale maziwa na mabwawa ya asili yaliyopo ndani ya nchi yetu yanatumiwa kwa matumizi kama hayo?

(b) Kwa kuwa Mkoani Singida tuna maziwa karibu 3 lile la Singidani na lile la Kindaya ambayo yako Singida Mjini, lakini Iramba tunayo Kitangiri. Napenda Mheshimiwa Naibu Waziri je, maji yaliyoko katika maziwa hayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu na umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la kuhusu mkakati wa Serikali kuhusu matumizi ya mabwawa, mito hali kadhalika tuliyonayo hapa nchini ambayo ni mingi mkakati wake ni upi.Kwa hivi sasa ni kwamba tuna programu hizi za sekta ya maji na programu hizi ni kwamba tumewapa jukumu Halmashauri zote za Wilaya ziibue na zibuni mbinu na aina ya miradi na teknolojia wanayoitaka. Kwa hali hiyo, basi ni jukumu la Halmashauri na ninapenda niwasisitize ya kwamba katika teknolojia ambazo zipo, ikiwemo maji chini ya ardhi, ikiwemo mabwawa na mito tunaomba wabuni miradi ambayo wailete na hiyo ndiyo ambayo itatekelezwa kwa sababu ni wenyewe ambao watajua kipi kinachofaa kwa wakati gani katika Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kuhusu mabwawa ya Kitangiri na mengine yaliyoko Singida, mimi nimetembelea Mkoa wa Singida na nimeona kuna mabwawa mengi na kwa mtu yeyote ukienda kwa haraka unaweza ukasema Singida imebarikiwa sana na mabwawa makubwa na mazuri. Lakini kwa bahati mbaya mabwawa yaliko Singida yote yana maji ya chumvi. Ni maji ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu. Kwa hali hiyo, basi kwa upande wa Singida na kwenye Halmashauri zao mbalimbali kwa hivi sasa wameomba miradi ya visima na miradi ya kutega maji ya mtiririko na hayo mimi ningeshauri kwamba ndiyo kwa hivi sasa yanafaa kwa ajili ya Mkoa wa Singida na ndio ambayo yataweza kuhudumia katika miradi mbalimbali na katika shughuli mbalimbali badala ya maji ya chumvi ya mabwawa ambayo yamezunguka Singida.

**MHE. ZUBERI ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye swali la msingi na hasa kipengele (a) na pamoja na uhusiano mzuri sana uliopo baina ya Tanzania na Malawi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatoa kauli gani kwa sababu tumekuwa tukipata jawabu kuhusiana na suala la mpaka baina ya Tanzania na Malawi ndani ya ziwa, wenzetu Malawi pamoja na uhusiano mzuri tulionao na wao mpaka hivi sasa wanaamini na wanajua na hata ramani zinazotolewa zinajua kwamba mpaka wa Tanzania na nchi hiyo, uko katika fukwe ziliko upande wa Tanzania. Tumekuwa tukipata majibu mbalimbali ya kujaribu kutatua tatizo. Je, ni lini ambapo tutakaa na wenzetu wa Malawi pamoja na uhusiano mzuri tulionao ili tuweze kutatua tatizo hili kwa sababu sasa hivi tunaona ni suala la uvuvi tu na maji. Kutakuja kujitokeza kitu kikubwa kituingize kwenye mgogoro usiokuwa wa lazima. Je, ni lini tatizo hili litatatuliwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**SPIKA:** Nisamehe Mheshimiwa Waziri, nadhani nilimwona pia Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, sasa kwa itifaki labda aanze yeye, halafu nitakupa nafasi na wewe umalizie. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir, ambalo nadhani amelielekeza Wizara ya Maji, lakini swali la mipaka tunaweza tukalijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania kwa kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tumekaa vikao viwili pamoja na nchi ya Malawi kuhusiana na suala hili la mgogoro wa mipaka.

Naomba kuwaambia WaheshimiwaWabunge kwamba hadi sasa hakuna mgogoro baina ya nchi hizi mbili na tunangojea kikao cha mwisho ambacho tutafuata sheria za kimataifa inayoelezea kwamba mipaka baina ya nchi mbili ambazo zinatenganishwa na maji unapita katikati ya ziwa lile au mapana katika bahari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maelezo ya ziada Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nadhani baada ya maelezo hayo ya kina ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ningependa kuongeza jambo moja tu kwamba maongezi haya pia yanawahusisha wenzetu wa Msumbiji pamoja na maelewano mazuri kati ya nchi yetu na Malawi na Msumbiji, ziwa hili linashirikisha Msumbiji, Tanzania na Malawi.

Tumekuwa na majadiliano na tayari tumeshasainiana mkataba (*memorandum of understandin)* mwaka 2004, wa maelewano ama MU pamoja na nchi ya Msumbiji. *(Makofi)*

Lakini harakati hizo zinaendelea kama alivyosema Naibu Waziri, wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ili tuwe na maelewano pia na nchi ya Malawi. Ahsante sana nashukuru. *(Makofi)*

Na. 132

**Mradi wa Maji na Benki ya *ADB***

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu imepata mradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa baadhi ya Vijiji lakini ubora miradi hiyo hairidhishi na kwa kuwa *ADB* hawaji kukagua miradi ili kujua maendeleo yake:-

Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya miradi ambayo haikutengenezwa vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Jimbo la Longido, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Monduli unatekelezwa katika Wilaya za Monduli na Longido kwa kutumia fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unalenga kuhudumia wakazi wapatao 109,000 katika vijiji 18 na miji midogo miwili. Mradi unatekelezwa katika mji mdogo wa Namanga, vijiji vya Eworendeke, Orkejuloongishu, Ngoswaki na Sinonik katika Wilaya ya Longido na Mji wa Monduli vijiji vya Alarsh, Mlimani, Lashaine, Meserani Juu, Loosimingori, Naiti, Makuyuni, Mswakini Juu, Oltukai, Losirwa, Majengo, Migombani na Barabarani Wilayani Monduli.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi ulianza tarehe 25/11/2005 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2008. Mradi umegawanywa katika kanda tatu ambapo kila kanda ina mkandarasi wake na kanda hizo ikiwemo Kanda ya Manyara, Kanda ya Kisongo na Kanda ya Longido. Ujenzi wa mradi hadi sasa ni asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa chini ya usimamizi wa Mhandisi Mshauri na Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Hivyo tatizo lolote la kiutekelezaji linapojitokeza hujadiliwa katika vikao vya Kamati ya kusimamia wa mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna miradi ambayo imejengwa chini ya kiwango alichopendekeza mtaalam Mshauri. Napenda pia kukiri ya kwamba utekelezaji wa mradi huu uliathirika kwa kipindi cha Novemba 2006 hadi Julai, 2007 kutokana na upungufu wa fedha kwa upande wa Serikali. Hata hivyo, hali hiyo sasa imerudi sawa na mradi unaendelea kutekelezwa vizuri na umefikia asilimia 75.

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Naogopa kubishana na Naibu Waziri. *(Kicheko*

Kwamba aliposema kwamba mradi umefikia asilimia 75. Labda nizungumzie upande wa Longido ambayo ninafahamu zaidi na ni jimbo langu. Vijiji alivyovitaja Kijiji cha Ngoswa na Kinaathnoneki, mradi haujaanza mpaka leo. Je, hivyo ndivyo vijiji anavyosema kwamba mradi upo kwenye asilimia 75 sehemu ambayo mradi bado haujaanza? *(Makofi)*

Pili, Kamati ya Ushauri nilitegemea kwamnba Kamati ya Ushauri wananchi husika nao wangekuwepo katika Kamati hiyo, lakini hawapo na mtu anayesimamia mradi huo ambaye nategemea yeye ndiye angetupa taarifa yuko Monduli. Je, Serikali itakubaliana nami kwenda kuangalia miradi hiyo kwa sababu wananchi wanateseka pamoja na kuwa na huo mradi mkubwa mpaka sasa hawajapata maji na maeneo ambayo yalikuwa na maji wameharibu miundombinu wananchi wamekosa maji? Naomba Serikali kama watakubaliana nami kwenda kuangalia miradi hiyo ili taarifa sahihi wailete Bungeni kuliko kusema taarifa ambayo siyo sahihi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sikumwona upesi, Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa majibu!!

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza kuhusu utekelezaji mdogo wa miradi kule Wilayani Longido, naomba nikiri kwamba kumekuwa na matatizo katika baadhi ya maeneo ya Longido ya utekelezaji wa mipango hii na hasa tatizo la msingi ni yale ambayo yanatokana na ucheleweshaji wa michango ya fedha za Serikali katika miradi hii.

Makubaliano kati ya *ADB* na Serikali yanahusiana pia na mchango wa fedha za Serikali katika miradi hiyo. Hiyo ilisababisha mwezi Novemba mwaka 2006 *ADB* walikataa kulipa fedha za wakandarasi kwa vile tulikuwa tumecheleweshа michango yetu.

Lakini Serikali kupitia Wizara yangu iliongea na *ADB* na waliruhusu kuendelea kulipia miradi hii baada ya kuweka ahadi kwamba tutachangia na katika Bajeti hii tumeweka fedha kwa ajili ya kuchangia. Kwa hivyo miradi ile iliathirika kwa kiasi fulani Wilayani Longido na pia Wilayani Monduli lakini hasa Longido.

Kuhusu kutembelea miradi ile nina uhakika Mheshimiwa Laizer hatojali kumpokea Mheshimiwa Naibu Waziri kuhakikisha anaiona hii miradi kwa karibu zaidi. Kamati ya Ushauri tutaiangalia, tumepokea tutaiangalia na tutaangalia namna ya kufanya maboresho kama itahitajika. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 133

**Muundo wa Bunge katika Kutunga Sheria na Kuridhia Maazimio**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba, mambo yote yanayoamuliwa na Bunge yanahusu masuala ya Muungano na kwa kuwa, kama Wizara Nne za Muungano, yaani Wizara ya Fedha, Mambo ya Nje, Mambo ya Ndani ya Nchi, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara nyingine si za Muungano:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, sasa ipo haja ya kuainisha upya Muundo wa Bunge na ushiriki wa Wabunge katika kutunga sheria na kuridhia maazimio kikatiba ili

kutoa fursa kwa Wabunge kutunga Sheria zenye kutumika pande zote mbili za Muungano badala ya sheria hizo kutumika katika upande mmoja tu wa Muungano?

(b) Wakati Serikali ikijibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, hapo tarehe 16 Aprili, 2007 ilisema kuwa swali hilo si la Muungano bali ni la Pemba. Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

(c) Je, ni nini kifanyike sasa katika kurekebisha hizo kasoro zisizo za msingi zinazoendelea kujitokeza mara kwa mara?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Busega, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977. Kwa mujibu wa Ibara ya 34 ya Katiba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatekeleza majukumu yanayohusu masuala ya Muungano na masuala yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara. Ibara ya 64 (4) inafafanua masharti ya kutunga sheria zinazotumika katika Jamhuri ya Muungano, yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kwa mujibu wa masharti hayo, sheria inayotungwa hutumika pande zote za Muungano ikiwa ni:-

(i) Sheria husika imetamka kuwa itatumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar;

(ii) Sheria hiyo inabadilisha au kurekebisha au kufuta sheria iliyokuwa inatumika zamani Tanzania Bara ambayo pia ilikuwa inatumika Tanzania Zanzibar; au

(iii) Sheria hiyo inahusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) na (3) ya Katiba, Bunge ni chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kina madaraka, kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake, yanayohusu masuala ya Muungano na yasiyohusu Muungano.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana . Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri mimi sielewi kama ameweza kujielekeza kwenye swali langu kama ambavyo nimeuliza kwa sababu mimi nilitaka kuuliza kwamba muundo wa Bunge ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa sababu ndani ya Bunge lako tumesikia mara nyingi majibu ya kutoka kwa Mheshimiwa Waziri akisema kwamba hilo ni swali la Pemba hilo ni la Zanzibar, si la Muungano. Sasa ina maana kuna Wabunge ndani ya Bunge hili ambao wapo kwa ajili ya kutunga sheria za

Wizara nne tu, hata Wizara ya Katiba hawashiriki, Wizara ya Afya hawashiriki. Wizara ya Miundombinu hawashiriki, sasa swali langu ni kwamba kwa nini Serikali isije na mfumo ambao utaainisha vizuri zaidi muundo wa ushiriki wa Bunge ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, ni kwamba Katiba ni *document* hai *is a leaving document*, inapaswa iwe inabadilika kadri ya mahitaji ya jamii inayohusika. Kwa maana ya kwamba kunakuwa na marekebisho mbalimbali na vizazi sasa hivi Tanzania vinaongezeka kila kukicha. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwa na mfumo rasmi wa kujaribu kuelimisha masuala mazima ya Kikatiba katika jamii ya Watanzania? Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la kwanza. Ni kweli mpaka sasa ni Wizara nne ambazo ni za Muungano na ni kweli kwamba kwa mujibu wa Katiba kuna masuala ya Bara na masuala ya Tanzania Visiwani, na Tanzania Zanzibar, ahsante kwa kunisahihisha na kama ndivyo ilivyo kwa mujibu wa Katiba itabidi tuendelee hivyo, kama alivyoomba kwamba Katiba irejewe na kama muafaka utapatikana basi tutafanya hivyo.

Kuhusu swali la pili, Mheshimiwa Spika, ni kweli, Katiba ni hai na inabadilika pale ambapo inahitajika na ni kweli vile vile tumekuwa tukiifanyia marekebisho Katiba yetu ingawa kwa sababu ni Sheria Mama mabadiliko haya lazima yawe makubwa. Kwa hiyo, kwa wakati muafaka tunapenda kuchukua ushauri wa Mheshimiwa Dr. Chegeni.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi wa Bara na Visiwani, kwa kuwa ndani ya Bunge hili kumeshatokea malalamiko kuhusu muundo na hata masuala yanayohusu muungano pande zote mbili na kwa kuwa Katiba inapaswa kujibu matatizo hayo yanayolalamikiwa na Wizara ya Mheshimiwa Waziri ndiyo inayotakiwa kuanzisha mchakato.

Je, Waziri atakubali kwamba sasa ili kuweza kupata ufumbuzi wa matatizo hayo Wizara yake itakuwa tayari kuanzisha mjadala wa kitaifa ili hatimaye Katiba mpya iweze kujadiliwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba nielezee Bunge lako Tukufu kwamba kuna mambo mawili hapa ya kufanyia rekebisho Katiba yetu pale ambapo inahitajika na suala la Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo nguzo kuu ya amani iliyopo na kwa kiasi kikubwa inatosheleza matakwa ya Watanzania. Lakini ninakubaliana na kama alivyouliza swali la pili la nyongeza Mheshimiwa Chegeni, pale ambapo marekebisho yanahitajika katika Katiba hii mzuri ambayo imehimili amani ya Watanzania hatutasita kufanya hivyo. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yametoa ufafanuzi nzuri katika Bunge hili. Lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba baadhi ya kero hivi sasa zipo hapa Tanzania za Muungano atakubaliana nami kwamba kero hizi zikifanyiwa haraka zikiondoka, zitaondosha matatizo yote haya ya kuzungumzia habari ya Katiba?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, napenda kuhamkikishia Mheshimiwa Hafidh Ali kwamba Serikali ya Muungano inajitahidi sana katika kuangalia kero ambazo zipo na kupatia ufumbuzi mara kwa mara. Nikitoa mfano, tulikuwa na tatizo la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kufanya kazi Zanzibar. Lakini kero ile imeondolewa na sasa hivi Tume inafanya kazi Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Ninaamini na kero zingine vile vile zitaondolewa hivyo ili moja hadi nyingine tuwe tumeondoa na kusiwe na sababu ya kuhoji Katiba yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata lilikwishajibiwa na aliyeuliza swali Mheshimiwa Machimu ameridhika. Kwa hiyo, tunahamia Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko swali linaulizwa na Mheshimiwa John Paul Lwanji.

Na. 135

**Mfumuko wa Bei ya Saruji**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu nchi za jirani Burundi, Rwanda, *DRC*, Malawi na Zambia, zimekuwa zikinufaika na biashara ya saruji kutoka Tanzania na katika muda huo hakukuwa na mfumuko wa bei ya bidhaa hii muhimu:-

(a) Je, Serikali ina habari kwamba mfumuko huu wa bei unatokana zaidi na upungufu bandia wa saruji yetu kwa kuwa sehemu kubwa inapelekwa Afrika Kusini kwa ajili ya Kombe la Dunia 2010?

(b) Kama hivyo ndivyo. Je, wananchi wetu wasitishe ujenzi wa nyumba bora hadi hapo michezo hiyo itakapokwisha?

(c) Je, wawekezaji katika viwanda vya saruji hapa nchini wana nia ya kuboresha Maendeleo yetu au wanavutia zaidi maslahi yao?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mhesimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hali halisi ya juu ya uzalishaji pamoja na soko la saruji hapa nchini umebainika kuwa jumla ya tani 1,575,756 huzalishwa na viwanda vilivyopo nchini kwa mwaka. Kiasi hicho kikilinganishwa na mahitaji ya nchi yanayokisiwa kuwa tani 1.3 milioni kwa mwaka uzalishaji huo ungeweza kutosheleza mahitaji ya nchi kwa kiasi kikubwa. Lakini uchambuzi huo pia umebainisha kuweko kwa ongezeko kubwa la saruji inayosafirishwa kwenda nchi jirani zikiwamo zile alizozitaja Mheshimiwa Mbunge; ambapo bei ya kuuzia saruji ni kubwa ikilinganishwa na bei za saruji hapa nchini. Kwa mfano, mfuko wa kilo 50 wa saruji unauzwa T.Shs.32,000 mjini Lubumbashi ikilinganishwa na T.Shs. 12,000 hapa nchini. Serikali inazo taarifa pia kwamba kiasi fulani cha saruji kinasafirishwa kwenda Afrika ya Kusini kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya michezo na majengo mbalimbali kwa ajili ya Kombe la Dunia mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini pia kumekuwepo na ongezeko la haraka la matumizi ya saruji kufuatia kuanzishwa kwa miradi mingi ya kitaifa inayoendelea kutekelezwa ikiwemo ya ujenzi wa shule, hospitali, madaraja ya barabara, mahoteli, viwanda pamoja na kasi kubwa ya ujenzi wa nyumba za wananchi binafsi. Kwa hiyo ongezeko kubwa la mahitaji ya saruji ndani na nje ya nchi linasabisha mawakala kuhodhi saruji hali ambayo inatoa mwanya kwa wafanyabiashara kupandisha bei. Serikali imebaini pia mawakala wa saruji wanaowauzia kwa wingi wafanyabiashara wanaosafirisha saruji kwenda nje bila kuzingatia taratibu na hivyo saruji hiyo kusafirishwa nje bila uhalali.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa saruji, Serikali imechukuwa hatua ya kidharura kwa kuruhusu uingizaji wa saruji kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki bila ushuru wa forodha ili kuhamasisha wafanyabiashara kuagiza saruji kutoka nje kwa kipindi cha miezi sita kufidia upungufu uliopo. Vile vile wenye viwanda wameeleza kuwa wako katika harakati za upanuzi wa viwanda vyao kwa kusudi la kuongeza uwezo wa uzalishaji wa saruji ifikapo mwaka 2008/2009. Aidha, vyombo vya usalama na *TRA* zimejipanga kuimarisha udhibiti ili kuhakikisha kuwa saruji inayouzwa nje ni ile iliyoruhusiwa kihalali.

Mheshimiwa Spika, suluhisho la kudumu la tatizo la upatikanaji wa saruji na upandishaji bei kiholela ni kuongeza viwanda vipya vya saruji, mpango ambao Serikali inaendelea nao kwa kuhamasisha wawekezaji wanaoweza kujenga viwanda vya saruji nchini kufanya hivyo.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Katika taarifa yake kwa umma Mheshimiwa Waziri kwenye mwezi wa tisa alituarifu kuhusu tatizo la upungufu wa saruji na kwamba alitaja nchi za jirani kadhaa na hizi nadhani ni hizi zote zinazotuzunguka isipokuwa Afrika ya Kusini. Sasa ilileta *speculation* kubwa sana watu wanazungumza kwamba saruji nyingi inakwenda Afrika ya Kusini kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya mpira.

Sasa ni sababu zipi Waziri hakuitaja, au hakueleza sababu hizo za Afrika ya Kusini kuchukua sehemu kubwa ya saruji yetu kwenda huko?

Pili, Mheshimiwa Spika, inasemekana kwamba saruji yetu ni bora na ndiyo maana inapendwa sana na nchi jirani na inavyoonekana kwamba kutakuwa na fidia ya kufidia hili pengo la upungufu kutoka nchi zingine. Sasa ningependa kuhakikishiwa kiwango cha saruji hiyo inayokuja kwetu hapa, na bei itakuwaje? Serikali inasema nini kuhusu hili? Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutokuitaja Afrika ya Kusini wakati tulipokuwa tunatoa taarifa huo mwezi wa tisa, mimi nadhani hata katika yale maelezo tulisema nchi kadhaa na leo hii katika jibu nimesema kwamba sasa Serikali inazo taarifa kwamba kiasi fulani cha saruji kinapelekwa huko Afrika Kusini. Sababu ya kusema kiasi fulani kwa sababu ni kama nilivyoeleza hapo katika majibu, baadhi ya saruji hii inasafirishwa kwa njia zisizo rasmi.

Kwa hiyo, kujua kiwango kama ni kikubwa au kidogo kwa kweli isingekuwa sahihi kuweza kuthibitisha hilo lakini taarifa hiyo Serikali inazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu ubora wa saruji itakayotoka nje. Serikali imejipanga na imejizatiti vizuri kwa sababu kati ya masharti ambayo yamekuwa katika uagizaji wa saruji kutoka nje ni pamoja na kuthibitishwa na Shirika letu la Viwango la *TBS* na vivyo hivyo kuzingatia ubora wake, bei ya saruji itakuwa siyo kubwa sana ukilinganisha na hii tunayoitumia hapa nchini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kulijibu swali hili na kutoa matumaini kwamba inawezekana saruji ikaja nchini kutoka nje lakini pia wenye viwanda wakapanua ujenzi wa viwanda hivyo.

Lakini mimi nataka nimwulize tu Mheshimiwa Naibu Waziri hivi kuna faida gani kujenga viwanda nchini wakati huo huo wananchi wazalendo wakakosa mbolea eti kwa sababu tu. Samahani sana nadhani suala la mbolea liko kichwani sana. Kwa hiyo, naomba unisamehe. Kuna faida gani basi kujenga viwanda vya saruji nchini wananchi wananchi hapa nchini wanaendelea kupata shida, eti kwa sababu saruji hiyo inatakiwa sana huko nchi za nje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza hapa ya kwamba saruji yetu inakwenda nje na hapa nchini vile vile kuna mahitaji makubwa zaidi yanazidi kuongezeka hasa katika hii miradi ya kitaifa ambayo inaendelea sasa hivi. Kwa hiyo. kuna upungufu.

Sasa upungufu huo lazima utafutiwe njia ya namna ya kuziba pengo hilo. Mojawapo ni hii ya kusema kwamba lazima tuagize kutoka nje kwa muda lakini

suluhisho la kudumu kusema kweli lazima tuongeze viwanda ili wananchi waendelee utoshelevu unaostahili. *(Makofi)*

Na. 136

**Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumeibuka ugonjwa wa kichaa cha mbwa katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Namtumbo, Kata ya Msindo na kwa kuwa watu watatu (3) wameshapoteza maisha yao kwa ukosefu wa dawa za kutibu ugonjwa huo:-

Je, Serikali itapeleka lini dawa za ugonjwa wa kichaa cha mbwa Wilayani Namtumbo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kichaa cha mbwa huenezwa na virusi ambavyo huingia ndani ya mwili wa binadamu kupitia jeraha linalotokea baada ya kuumwa na mbwa au mnyama mwingine mwenye ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Ugonjwa huu hauna tiba bali unaweza kuzuilika kwa kiasi kikubwa kwa kutoa chanjo muda mfupi baada ya mtu kuumwa na mbwa au mnyama mwenye ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Uwezekano wa kupona kwa mtu aliyeambukizwa hasa kama hakupata chanjo ya ugonjwa huu ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa tulizonazo kunako mwezi Februari na Septemba 2007 watu wawili kutoka vijiji vya Mkongo na Mtakanini Wilayani Namtumbo walifariki kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Hii ilitokana na kuchelewa kupata chanjo mara baada ya kuumwa na mbwa au mnyama anayehisiwa kuwa na ugonjwa huo. Mgonjwa wa kwanza aliumwa na mbwa mwezi Novemba, 2006 na kuripoti hospitali ya Mkoa Ruvuma mwezi Februari 2007, ambapo mgonjwa wa pili aliumwa na mbweha mwezi Julai 2007 na kuripoti hospitali mwezi Septemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara yangu hutoa chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vikiwemo vile vya

Namtumbo. Aidha, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo tumeandaa rasimu ya kutekeleza mpango wa kuchanja mbwa wote wanaofugwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wananchi wote kwamba mara wanapoumwa na mbwa au mnyama yeyote anayehisiwa kuwa na kichaa cha mbwa waripoti haraka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupatiwa chanjo ya kuzuia ugonjwa huo.

Aidha, naziomba Halmashauri kuwadhibiti mbwa wanaozurura hovyo katika makazi ya watu ili tuweze kupunguza matukio ya watu kuumwa na mbwa na hatimaye kupunguza ugonjwa wa kichaa cha mbwa nchini. Mwisho nawaagiza Waganga Wakuu wote katika hospitali za Wilaya na Mikoa kuhakikisha wanayo akiba ya kutosha ya chanjo ya kichaa cha mbwa ili kuwapatia wale watakaoripoti bila kukosa.

&&&&

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

(a) Kijiografia Wilaya ya Nantumbo, tuna misitu mingi sana na kila siku katika maisha yetu ya mashambani tunaishi na jamii ya mbwa inayoitwa Mbweha na inasemekana watu waliofariki vifo vyao vilisababishwa na mbwa hao aina ya Mbweha, je, Serikali inaweza kufanya utafiti ili kutambua ni kipindi gani mbwa huwa wanapata kichaa na kushauri wananchi wawe waangalifu kwa mbwa hao wa porini?

(b) Kwa kuwa, ni vigumu kwa Serikali kutoa chanjo kwa jamii hii ya mbwa wa porini, je, inaweza kuona umuhimu wa kuweka dawa hizi katika vituo vyetu vya afya vya Nantumbo kwa sababu watu hawa walipoumwa na mbwa hawa katika vituo hivyo kulikuwa hakuna dawa hizi za kichaa cha mbwa ?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hakuna utafiti wowote ulioonyesha au unaoweza kuonyesha kwamba kuna msimu maalum wa ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Ushauri ambao tunapenda kuwapa wananchi kama nilivyosema, mara waumwapo na mbwa au mnyama yoyote hata kama hana dalili za kichaa cha mbwa, ni kwenda mara moja katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupatiwa chanjo.

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba hakuna tiba bali kuna chanjo ya kuzuia ugonjwa huu wa kichaa cha mbwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba muda wa kujitokeza dalili za ugonjwa huu mtu anapoumwa na mbwa au mnyama yoyote ambaye ana ugonjwa huu wa mbwa, yaani *incubation period*, kwa kawaida huwa ni mrefu sana kulingana na sehemu ambayo ameumwa hivyo kumfanya pengine yule muumwaji wa mbwa akasahau hata lini aliumwa na mbwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kutoa taarifa kwamba tunazo dawa za chanjo za kutosha na kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge, kwa Mkoa wa Ruvuma tulishapeleka chanjo jumla ya vichupa 800 kuanzia tarehe 5 Februari 2007 mpaka tarehe 1 Novemba 2007.

Mheshimiwa Spika, napenda tena kutoa wito kwa kila Mganga Mkuu aliye katika hospitali yake, ahakikishe kwamba dawa hizi wanazo na pale zitakapopungua basi waende wakachukue kule Mkoani ili wahakikishe kwamba wanayo *stock* ya kutosha mara wananchi watakapofika katika vituo vyao ili waweze kuwapatia chanjo hizi.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, maradhi yote ya binadamu au wanyama yana chanzo chake, mfano malaria ni mbu, homa ya matende ni mbu, UKIMWI vile vile sababu sote tunazijua, je, ni nini chanzo cha maradhi ya kichaa cha mbwa? Ni sababu gani mbwa anapata maradhi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nilipokuwa najibu swali la msingi nimesema kwamba ugonjwa wa kichaa cha mbwa hutokana na virusi. Kwa maana hiyo, mbwa ambaye amepata uambukizo wa virusi hivi ambavyo vinaleta kichaa cha mbwa atakapomng’ata au kumuuma binadamu basi virusi vile vinaweza vikapenya katika jeraha na kuingia katika mwili wa binadamu na hivyo kupata virusi hivi vya kichaa cha mbwa. Kwa hiyo, naomba nisisitize kwamba tujihadhari, wale watakaoumwa na mbwa au mnyama yoyote yule, waende hospitali ili waweze kupata ufahamu zaidi na ushauri kutoka kwa wataalamu wa afya.

Na. 137

**Tatizo la Malaria Nchini**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI (K.n.y. MHE. OMAR ALI MZEE)** aliuliza:-

Kwa kuwa mbu aina ya *Anopheles* ni tishio kwa kusababisha malaria katika nchi za joto ikiwemo Tanzania:-

(a) Je, uhai wa mbu huyo ni siku ngapi?

(b) Je, ukiacha usafi wa mazingira na kutumia dawa, ni njia zipi zaidi zitumikazo kujikinga na maambukizo yatokanayo na mbu huyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mbu wa aina ya *Anopheles* anayeeneza ugonjwa wa malaria anaishi kwa wastani wa siku 14 hadi 21 kulingana na mazingira aliyopo mtu huyo.

(b) Mheshimiwa Spika, zaidi ya usafi wa mazingira na kutumia dawa, njia nyingine zinazotumika kujikinga na maambukizo yatokanayo na mbu waenezao malaria ni pamoja na kuangamiza mbu wapevu, kuangamiza viluwiluwi kwa kutumia viuatilifu *(larviciding)* na kuangamiza mazalia ya mbu.

Njia zinazotumika kuangamiza mbu wapevu ni pamoja na matumizi ya vyandarua vyenye viuatilifu *(Insecticide Treated Nets, ITNs)*. Serikali inatekeleza Mpango wa Hati Punguzo kwa kuwapatia vyandarua vya namna hii wanawake wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. Makundi haya mawili ndiyo yanaathirika zaidi na ugonjwa wa malaria. Njia nyingine ni kunyunyiza ukoko wa viuatilifu ndani ya kuta za nyumba *(Indoor Residual Spraying, IRS).*

Mheshimiwa Spika, njia zote hizi zinapaswa kwenda sambamba na ili ziweze kufanikiwa, tunahitaji kuwapo ushirikiano wa dhati kati ya sekta ya afya, sekta nyingine na jamii kwa ujumla. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kushirikiana na Halmashauri zao katika kuwahamasisha wananchi kuungana na Serikali katika mpambano huu ili kuhakikisha kuwa ugonjwa wa malaria unadhibitiwa kwa kufuata njia hizi.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, kwavile watu wetu katika nchi yetu ya Tanzania wanaangamia kwa maradhi ya malaria zaidi ya UKIMWI:-

(a) Je, kwanini hazifanyiki juhudi za makusudi za kuendelea kufanya *Indoor Spraying*, kunyunyuzia kuta za nyumba ili kuwaua mbu hao, kwa sababu juhudi hizi zinakwenda kwa kusuasua?

(b) Je, ni sehemu gani ya nchi yetu kwa mwaka uliopita wa bajeti imenyunyuziwa dawa hizi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, si kweli kwamba Serikali inasuasua katika kupambana au kupiga vita tatizo la malaria. Kumekuwepo na programu nyingi na sasa hivi kwa mfano Programu ya Kunyunyizia Dawa Zanzibar imefanikiwa vizuri sana kiasi kwamba idadi ya wagonjwa wanaoripoti Hospitalini kwa sababu ya malaria imepungua na sasa hivi Programu ya Taifa ya Kuzuia Malaria, inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, mwaka jana Muleba walipata tatizo kubwa sana la malaria na ilienda ikafanyiwa unyunyuziaji na sasa hivi Serikali inafanya maandalizi ili kuweza kuona kwamba tunafanya *Indoor Spraying* huku Bara yaani katika upande wa Bara ili kuhakikisha kwamba tunaua hivi viluilui na hatimaye kuweza kupunguza ugonjwa huu wa malaria.

Na. 138

**Asilimia 25 ya Fedha za Mapato ya Wanyamapori**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipojibu swali Na. 164, lililoulizwa na Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, ilisema kuwa, haitaongeza asilimia 25 ya fedha zinazotoka Hazina baada ya mapato kupatikana licha ya Idara ya Wanyamapori kuongeza mapato yake na kwa kuwa Serikali pia ilisema kwamba wenye vitalu wanasaidia miradi ya maendeleo kwenye maeneo husika:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa ufafanuzi wa kueleweka zaidi juu ya majibu hayo?

(b) Kama wenye vitalu wanasaidia miradi ya maendeleo kwenye maeneo yanayopakana na vitalu, je, Serikali haioni kwamba fedha zinazochangiwa hazina fomula maalumu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Ni kweli, katika jibu la swali Na. 164, la Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, tarehe 6 Julai 2006, Serikali ilisema kuwa haitaongeza asilimia 25 ya fedha zinazotoka Hazina kwenda Halmashauri za Wilaya zenye maeneo ya uwindaji wa kitalii. Aidha, Kanuni ya 10(4)(b)(i) ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2000 na marekebisho yake, inaelekeza kuwa kampuni za Uwindaji wa Kitalii zinatakiwa kuchangia shughuli za miradi ya maendeleo ya wananchi wanaoishi karibu na vitalu vya uwindaji, uzuiaji wa ujangili na uendelezaji wa vitalu.

Mheshimiwa Spika, mgao wa asilimia 25 ya fedha kwa Halmashauri za Wilaya hutokana na mgao wa fedha zinazopelekwa Hazina kutokana na ada za vitalu vya uwindaji wa kitalii na wanyamapori waliowindwa katika vitalu vilivyotengwa kwa shughuli za uwindaji wa kitalii. Sambamba na hilo, Wizara yangu imetoa mwongozo wa matumizi ya fedha hizo ambapo asilimia 60 ya fedha hizo zinatakiwa kusaidia miradi ya maendeleo ya wananchi kwenye vijiji ambavyo uwindaji unafanyika na asilimia 40 kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua ya Serikali ya kuongeza ada za vitalu vya uwindaji wa kitalii kutoka dola za Kimarekani 10,000 hadi dola za Kimarekani 50,000 kwa vitalu vya kundi A na dola za Kimarekani kutoka 10,000 kwenda dola za Kimarekani 40,000 kwa vitalu vya kundi B, vilevile kutokana na ongezeka la ada za uwindaji wa kitalii mfano tembo toka dola za Kimarekani 5,000 hadi 15,000 simba na chui toka dola za Kimarekani 2,5000 hadi 12,000, ni dhahiri kuwa mapato yataongezeka.

Aidha, ni wazi kuwa fedha itakayopelekwa Halmashauri kwa kuzingatia mgao wa asilimia 25 kutokana na mapato ya uwindaji wa kitalii, zitaongezeka vilevile.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kiwango cha michango inayotolewa na Makampuni ya Uwindaji wa kitalii katika miradi ya maendeleo ya wananchi, kila kitalu hutakiwa kuchangia si chini ya shilingi 1,203,825 kwa mwaka utaratibu ulioanza tangu mwaka 2000. Kiwango hiki cha kuanzia kilitokana na wastani wa michango iliyokuwa ikitolewa na kampuni za uwindaji kwa kila kitalu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mahitaji ya maendeleo ya wananchi, kampuni za uwindaji wa kitalii zimekuwa zikichangia zaidi ya kiwango hicho katika shughuli za ujenzi wa vyumba vya madarasa, majengo ya ofisi za vijiji, zahanati, uchimbaji wa visima vya maji, ununuzi wa madawati, madawa ya binadamu na kadhalika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, anaweza kuliambia Bunge hili:-

(a) Taarifa kutoka kwenye zile Wilaya ambazo zinatumia fedha hizi zinarudi Serikalini ili kujua kama zinatumika vizuri?

(b) Kwa kuwa fedha hizi zinachelewa sana kwenda kwenye Wilaya husika, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuhakikisha kwamba fedha hizi zinakwenda kwa wakati ili ziweze kufanya kazi zilizokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na taarifa, Halmashauri huwa zinarudisha taarifa ya matumizi ya pesa ambazo wamepata kutokana na mgawo wa asilimia 25. Pesa zinazotolewa ambazo ni asilimia 25 kama mgawo wa mapato, huwa mpaka uwindaji wa kitalii ukamilike. Kipindi cha uwindaji wa kitalii huwa kinaanza Julai mpaka Desemba 30 na mapato mpaka yarudishwe Hazina, ndipo pesa hizo zinapelekwa tena kwenye Halmashuri. Lakini hata hivyo, tumepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge, tutajitahidi kuzipeleka mapema iwezekanavyo.

Na. 139

**Ufufuaji wa Vituo vya Kuzalisha Umeme Nchini**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa tumeshapata vipindi viwili vya shida kubwa ya nishati ya umeme, hasa kipindi cha mwaka 2006 na kwa kuwa hatujui hali itakuwaje miaka ijayo kutokana na mambo ya *"Global Warming"*:- Je, Serikali ina mikakati gani ya kuvifufua vituo vidogo vidogo vilivyokuwa vikizalisha umeme siku za nyuma katika baadhi ya maeneo hapa nchini kama kituo cha Kikuletwa kilichopo Kata ya Masama Rindugai, Wilayani Hai

ambapo kuna taarifa kituo hicho kikikarabatiwa kinaweza kuzalisha *"in series"* hadi *20 MW*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatia Shirika la *TANESCO* kupokea maombi kutoka kwa baadhi ya kampuni binafsi zenye nia ya kufufua vituo vidogo vya kuzalisha umeme wa maji vya Kikuletwa, Tosamaganga na Mbalizi ambavyo viliachwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, mwezi Machi 2003, Shirika la *TANESCO* lilichukua hatua ya kutangaza zabuni ya kufufua vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya zabuni ilionyesha kwamba bei za umeme zilizokuwa zinapendekezwa na wazabuni zilikuwa za juu ambazo zingesababisha Shirika la *TANESCO* kununua umeme kwa hasara. Kutokana na mazingira ya sasa kuwa tofauti na ya wakati ule ambapo ilionekana ni vigumu kwa *TANESCO* kuingia mikataba na wazabuni waliojitokeza, sasa Srikali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo *TANESCO,* inaandaa utaratibu mzuri kwa kutayarisha mikataba ya msingi ya kununua na kuuziana umeme pamoja na upangaji wa bei za umeme yaani *standardized small power purchase agreements and power purchase tarrifs,* kwa miradi midogo ya umeme itakayokuwa inauza umeme *TANESCO* kupitia kwenye gridi na nje ya gridi. Lengo kubwa, ni kuboresha na kurahisisha kampuni binafsi ili ziweze kushiriki katika miradi midogo midogo ya umeme kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme pamoja na kuongeza kasi ya kuwapelekea wananchi wengi wa mjini na vijijini huduma ya nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika utaratibu niliouelezea hapo juu, *TANESCO* watatangaza tena tenda ya kupata kampuni bora ambazo zitaendeleza vituo vya Kikuletwa, Tosamaganga na Mbalizi ili viweze kuchangia ipasavyo maendeleo ya sekta ndogo ya umeme. Aidha, mchakato wa kutunga Sheria mpya ya Umeme utakaoruhusu sekta binafsi kutoa huduma ya nishati, unaendelea.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ki-*digital* lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, katika jibu lake la msingi amesema kwamba hii Sheria mpya ya Umeme itakayoruhusu sekta binafsi kutoa huduma ya nishati inaendelea, ningependa niulize:-

(a) Je, ni lini hiyo sheria itaweza kuwasilishwa hapa Bungeni mapema iwezekanavyo kwa kutambua kwamba kuna mahitaji makubwa ya umeme kutokana na viwanda vinavyojengwa na vitakavyoendelea kujengwa hapa nchini siku za karibuni?

(b) Kwa kuwa, ni nia na lengo la Serikali kusambaza umeme katika maeneo mengi kadri inavyowezekana na kwa kuzingatia katika baadhi ya maeneo yetu ya Wilaya ya Hai, umeme umeshapita, huu wa *11 KV*, je, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa haraka kwa maana ya kuhakikisha kwamba usambazaji wa umeme katika yale maeneo ambako umeme mkubwa umeshapita kule Wilayani Hai utapatikana mapema kadiri iwezekanavyo, kwa mfano katika vijiji vya Mungushi, Hai Mjini, Mwadiwa na kwingineko ili wale wananchi waweze kupata huduma hii muhimu ya umeme na Shirika la *TANESCO* liendelee kupata mapato?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwenye swali la kwanza kuhusu sheria, nadhani tumeshalitolea taarifa wakati wa ufunguzi wa Mkutano huu wa Bunge. Tulisema kwamba Sheria ya Umeme itawasilishwa Bungeni na suala hili linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kufikisha huduma ya umeme kwenye maeneo ambayo umeme wa msongo mkubwa umepita katika Wilaya ya Hai, napenda kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, nimuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi *TANESCO* inaendelea na mchakato wa kuona ni jinsi gani tunaweza kufikisha huduma hiyo kwenye maeneo hayo. Tumewasiliana na *TANESCO* Wilaya ya Hai na hata leo asubuhi tumewasiliana nao, taarifa sasa hivi ziko Makao Makuu ya *TANESCO* kwa ajili ya kuona ni jinsi gani utekelezaji ufanyike na ufanyike kwa hatua zipi na ni lini uanze. Lakini kimsingi, sasa hivi tayari hatua zinaendelea kuchukuliwa kwa ajili ya kuwafikishia wananchi wa maeneo hayo huduma ya umeme.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, ni vigumu kujua athari za *global warming* na hasa kuhusiana na upatikanaji wa umeme, kitu ambacho tumejifunza hapa Tanzania hivi karibuni, je, Wizara ina vyanzo vipi ambavyo inavipa vipaumbele kwa ajili ya kuzalisha umeme na kwa umuhimu upi, *proportionality,* kwa kujikinga au kujiweka sawa na lolote litakalokuja kutokana na *global warming?* Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kufuatana na matatizo ya ukame uliotupata hapa Tanzania, sina hakika kwamba ni kwa sababu ya *global warming*, lakini tunaweza kuiweka katika njia hiyo. Tuliamua kwamba tutapanua wigo kwa vyanzo vyetu vya umeme. Kwanza chanzo kikubwa ambacho tutaendelea kukitegemea ni cha umeme wa maji kwa sababu kufuatana na gharama za uzalishaji, ndio umeme ambao uko nafuu kabisa. Lakini chanzo cha pili ambacho kwa umuhimu kwa *percentage* kwa sasa hivi hatuna lakini tunaweza kumpatia cha pili kwa kufuatilia itakuwa ni umeme unaotumia gesi. Kwa sababu tayari mashine za vyanzo vya gesi tunazo hapa. Lakini cha tatu itakuwa ni kuendeleza rasilimali yetu ambayo ni umeme kutokana na makaa ya mawe. Sasa hivi tutakuwa na mkataba wa kuendeleza Kiwira lakini vile vile tunajua katika Jimbo lake kuna Mchuchuma na yenyewe tunaiangalia kwa njia hiyo hiyo.

Mheshimiwa spika, lakini kuna vyanzo vingine vya umeme vya vidifu kwa mfano kama hii *wind power*, ambapo na vyenyewe tunaifanyia utafiti pamoja na *mini hydros* kama alivyozizungumzia Mheshimiwa kwenye swali lake la msingi. Nafikiri ndivyo

tunavyofanya, lakini kwa takwimu, kwa *percentage* kiasi gani, itakapotoka ile *power master plan* ndio tutaweza kuviangalia ambayo tunafikiri itatoka wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelijibu vizuri, ni juu ya Sheria hii mpya ya Umeme kwamba itakuja lini. Nafikiri kama mtakumbuka kwenye Bunge lako, kwenye kikao chako hiki, Muswada huu umekwishasomwa kwa mara ya kwanza. Kwa hiyo ina maana sasa hivi hiyo sheria imekwishakuwa *public* na walisema vile vitabu mtavikuta kwenye *pigeon holes* zenu. Kwa hiyo, tuna uhakika mambo yakienda sawa tunategemea kuuleta katika Bunge litakalokuja la mwezi wa pili, ahsante sana.

Na. 140

**Ulipaji Fidia kwa Ardhi na Mali za Wananchi**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Umeme (*TANESCO)*, limekuwa likichukua ardhi na mali za wananchi ili kupitisha njia za kusambaza umeme na kwa kuwa, Shirika limekuwa likiwapa wananchi hao fidia ndogo zisizolingana na thamani ya mali zinazoathiriwa licha ya Sheria ya Ardhi kubainisha wazi juu ya namna ya kuwafidia watu hao:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa adhabu kali kwa watu waliopewa dhamana ya kusimamia zoezi la kuthamini mali za wananchi kwa niaba ya Shirika lakini wanafanya zoezi hilo kwa upendeleo na bila kufuata sheria na kanuni zilizopo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuiamrisha *TANESCO* kulipa tofauti ya fidia pale itakapobainika kwamba baadhi ya wananchi wamepunjwa katika zoezi la ulipaji wa fidia kwa ardhi na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* linapotaka kupitisha miundombinu yake katika eneo lolote, kwanza huwasiliana na Wizara ya Ardhi ili kumpata mtaalam wa kuthamini ardhi na mali za wananchi zitakazoathiriwa kwa ujenzi wa miundombinu husika. Baada ya Mthamini kukamilisha kazi ya uthamini na kupitisha taarifa yake katika ngazi za uongozi wa Serikali kutoka kijiji hadi Mkoa, huwasilisha taarifa hiyo *TANESCO* kwa ajili ya kuandaliwa malipo. *TANESCO* huandaa malipo kulingana na tathmini iliyofanywa na Mthamini wa Serikali na malipo ya fidia hufanywa katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la *TANESCO* hulipa wananchi fidia ya ardhi na mali zinazoathiriwa na ujenzi wa miundombinu kulingana na tathmini iliyofanywa na Mthamini wa Serikali. Wakati wote, Serikali iko makini kuhakikisha kwamba tathmini hazifanywi kwa upendeleo na wala hazikiuki sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, inapobainika na kuthibitika kuwa wapo baadhi ya wananchi wamepunjwa katika zoezi la ulipaji fidia wa ardhi na mali zao, *TANESCO* bila kusubiri kuamrishwa na Serikali huwajibika kuwasiliana na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kupitia upya taarifa ya uthamini na ikibidi kurudia zoezi la uthamini na hatimaye kulipa tofauti inayobainika.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa, mchakato mzima wa kutathmini mali za wanaoathirika na miradi hii ya *TANESCO* huwa hawawashirikishi wananchi hawa kikamilifu, kinachofanyika ni katika hatua za mwisho kabisa kuwaambia saini hapa, chukua cheki yako, ondoka. Je, Serikali haioni sasa kuna haja kabisa ya kuwashirikisha wananchi katika hatua zote wakati wa kutathmini mali zao?

(b) Endapo itathibitika kwamba kuna baadhi ya wananchi ambao mali zao zimechukuliwa na fidia waliyopewa ni ndogo sana, je, Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano wa karibu kuhakikisha kwamba watu hao wanapewa fidia yao haraka iwezekanavyo ili waweze kuandaa makazi mapema kabla zoezi la bomoabomoa halijawafikia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, jinsi gani wananchi wanavyoshirikishwa katika mchakato, niseme tu kama tulivyowaeleza kwenye jibu la msingi, wananchi wanashirikishwa lakini tunaheshimu maoni na kauli ya Mheshimiwa Mbunge, inawezekana katika uzoefu wake na pia uzoefu wa Waheshimiwa wengine kuna mahali ambapo kumejitokeza kasoro lakini kama nilivyothibitisha kwenye jibu la msingi, panapojitokeza kasoro Serikali ipo tayari kusikiliza na kutatua kasoro hizo kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwamba endapo itathibitika kwamba wananchi wamelipwa kidogo sana, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali ipo makini kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao na stahili zao kwa mujibu wa sheria. Kwa hivi ni jambo la kawaida kwamba endapo kutajitokeza kasoro yoyote ile, Serikali itaendelea kusikiliza na kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni pia tulikuwa tunashughulikia suala la ulipaji wa fidia kule Rufiji kulikuwa na kasoro ambazo zilijitokeza lakini tumeendelea kuzibaini na sasa hivi tuko kwenye hatua za mwisho kutatua kasoro hizo. Kwa hiyo, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba tuko tayari mahali popote ambapo panajitokeza kasoro, watupe taarifa ili tuendelee kutatua kasoro hizo.

Na. 141

**Kuboresha Kilimo cha Mpunga**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo kubwa la kilimo cha mpunga katika Wilaya za Kilombero na Ulanga ni namna bora ya upandaji mpunga na upatikanaji wa mbegu bora iliyofanyiwa utafiti wa kutosha:-

(a) Je, Serikali inaweka mkakati gani wa makusudi ili kuhakikisha wakulima wa mpunga wa Wilaya hizo wanapanda mbegu kitaalamu kuliko kutumia njia ya asili ya kumwaga mpunga *(broadcasting)*?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka Maofisa Ugani kwenye maeneo hayo ili elimu ya kilimo bora itolewe mashambani kwa wakulima kuliko elimu hiyo kuishia kwenye shamba darasa?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kutumia Mfuko wa Pembejeo kuwakopesha wakulima hao *power tillers* na *planters* za mpunga?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekwishatoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kuandaa mkutano au kongomano pamoja na Wabunge ili tuweze kujadili kwa pamoja mfumo ambao utafaa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa mbolea. Wale waliokuwa wanajua kwamba tungeufanya kesho, naomba niseme kwamba kwa ajili ya maandalizi, tumeuahirisha, hatutaufanya kesho lakini tutawatangazia ni lini tena ili uweze kuwa wa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka utaratibu wa kuwapatia wakulima mafunzo kwa kutumia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa. Utaratibu wa Shamba Darasa, una lengo la kuwawezesha wakulima kujifunza kanuni za kilimo bora kuanzia kutayarisha pembejeo, kuandaa mashamba, kupanda, kutunza mazao mashambani hadi kuvuna wakiwa mashambani, kwa ushirikiano wa karibu baina yao na wataalamu wa kilimo. Wakulima wanaohitimu katika mafunzo ya Shamba Darasa wanatakiwa kuwa chachu kwa wakulima wengine ili nao wajifunze kanuni hizo. Hii itasaidia mafunzo haya yasiishie kwenye mashamba ya mafunzo bali yaende hadi katika sehemu za uzalishaji mashambani.

Katika Mkoa wa Morogoro, wataalam wawili kutoka katika kila Wilaya wamepatiwa mafunzo juu ya upatikanaji wa mbegu bora ya mpunga iliyofanyiwa utafiti na namna bora ya upandaji wa mpunga. Wataalam hawa watawafundisha wataalam wengine katika ngazi ya Kata na Vijiji ili mbinu hii iweze kusambaa kwa wakulima wengine.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka Maofisa Ugani Vijijini, Serikali imejiwekea mpango wa kuwa na Wataalam wa Ugani katika kila kijiji, Kata na Tarafa ifikapo mwaka 2010/2011. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali itaajiri wataalam 2,500 katika mwaka wa fedha 2007/2008 kupitia TAMISEMI. Utaratibu wa kuajiri wataalam 11,703 pengo la uhaba wa wataalam litakuwa limezibwa katika kipindi hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo unatoa mikopo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji katika sekta ya kilimo na mifugo. Mikopo hiyo ni kwa ajili ya pembejeo za kilimo, ununuzi wa matrekta mapya, ukarabati wa matrekta yaliyoharibika, mikopo ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta, mikopo ya kununua matrekta madogo *(power tillers)*, zana za kukokotwa na wanyamakazi, pampu za umwagiliaji na mashine ndogo za kusindika mazao. Walengwa ni wakulima binafsi, vikundi vya wakulima vilivyosajiliwa kisheria hasa katika skimu za umwagiliaji, Vyama vya Ushirika vya Msingi, Mifuko ya Pembejeo ya Wilaya na *SACCOS.* Kufikia Septemba, 2007, Mfuko wa Pembejeo umekwishatoa mikopo kwa ajili ya kununulia matrekta 52 katika Wilaya ya Mbarali na trekta moja moja katika Wilaya za Mvomero na Songea.

Mheshimiwa Spika, inaonekana wakulima wengi hawajauelewa Mfuko wa Pembejeo. Wizara yangu imeuagiza Mfuko huo kujinadi kwa walengwa kupitia katika Halmashauri za Wilaya ili wakulima waelewe vizuri mchakato wa kupata mikopo na masharti nafuu yaliyomo. Lengo ni kuondokana na jembe la mkono, kuongeza tija na kupunguza harubu kwa mkulima.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa jitihada zake za kufufua kilimo katika nchi hii kwa sababu bila ugani kilimo hakiwezekani. Pamoja na pongezi hizo, nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Rais Kikwete, alishasema kwamba angependa Mkoa wa Morogoro uwe ghala la Taifa ikiwa pamoja na kuendeleza zao la mpunga na kwa kuwa katika Mkoa huo kuna shamba la mpunga la Kotako au Kihoko katika Tarafa ya Mgeta, lilikuwa linalima mpunga na limekuwa *disgned* kwa kulima na kwa kuwa wawekezaji wenye uzoefu wa kulima mpunga walishapatikana tangu mwezi Juni mwaka huu, je, Serikali haioni kuwa hawa wawekezaji kwa kukaa muda wote huo kungojea uamuzi wa Serikali ni kuchelewesha maendeleo ya wananchi wa Tarafa hiyo ya Mgeta kwa vile wao ni wakulima wa mpunga na wameahidiwa kwamba watawekewa miundombinu ya umwagiliaji kama wao watakavyoweka shamba kwao?

(b) Wawekezaji hao pamoja na kutuahidi kutuwekea miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba yetu wale tunaozunguka shamba lile la Kihoko, wametuahidi vilevile kutuletea umeme jambo ambalo mimi nimeliomba zaidi ya mara sita hapa Bungeni lakini sijawahi kupata, wametuahidi kuboresha barabara yetu kutoka Ifakara mpaka Mgeta…

**SPIKA**: Mheshimiwa, ni maswali si hotuba, ni maswali.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Kwa kuwa wametuahidi kutujengea sekondari, hizo zote ni kwa kuwa, swali linakuja je, kwa kuchelewa au kutotoa uamuzi juu ya hawa wawekezaji, haoni kwamba Serikali itakuwa inawanyima haki za msingi hawa watu ambao wameahidiwa vitu vya kimaendelea ambavyo Serikali haiwezi kuwapatia?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali mawili makubwa ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Ligallama, napenda kwanza kutumia fursa hii kutoa rambirambi zangu kutokana na kifo cha Mbunge mwenzetu, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Mbatia. Natoa rambirambi hizo sasa hivi kwa sababu ndiyo mara yangu ya kwanza kuzungumza hapa Bungeni tangu msiba huo ulipotokea.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kwa kunichagua kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu maswali mawili makubwa ya Mheshimiwa Ligallama, kwanza kuhusu shamba la Kotako, Serikali haikucheleweshwa chochote. Ninapenda nimfahamishe kwamba Serikali imeshafikia uamuzi na mwekezaji amesharuhusiwa na mamlaka husika kuendeleza bonde la Rufiji yaani Lubada na imeshaarifiwa juu ya uamuzi huo wa Serikali.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Ligallama pamoja na wananchi wa Kilombero washirikiane na mwekezaji aliyekubaliwa, katika kuendeleza Tarafa hiyo na hivyo kutekeleza ahadi ambazo zilikuwa zimekwishawekwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi wa eneo hilo huduma za barabara na vilevile kuwawezesha kupata mifereji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha mpunga. Nadhani Mheshimiwa Ligallama sasa atakuwa tena hana matatizo juu ya jambo hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita kabisa. Tuna swali moja tu ambalo limesalia la Mheshimiwa James Daudi Lembelii, tutalipangia siku nyingine.

Matangazo, nikianza na wageni, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busenga, anao wageni wake na naomba ninaowatamka wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Wageni hawa wako wanane na wanatoka nchini Norway wakiongozwa na Mama Anna Maria Lifolu ambaye ni Katibu Mkuu wa akinamama wa *Centre Party* kule Norway. *We feel happy to welcome you to* Dodoma *and particularly to the Parliamentary Chamber of Tanzania. Our visitors from Norway, you have come a long way, we as a nation we are very close to Norway because Norway is very good development partner. It is a pleasure to have you with us here in Parliament, feel at home. Please, you may sit down.*

Waheshimiwa Wabunge, hawa Wajumbe wanane baadhi yao wakiwa ni Wabunge kutoka Chama hicho cha *Center Party*, ni sehemu ya Mradi Shirikishi wa Haki na Demokrasia ambao wanashirikiana na Wilaya hiyo ya Magu. Kwa hiyo, wako wenzao kutoka Magu ambao ni wageni 34 wakiongozwa na Ndugu Samweli Ibambasi, Mratibu wa Mradi wa Demokrasia, naomba wasimame wageni kutoka Magu. (*Makofi*)

Mradi huu wa Haki na Demokrasia, unaendeshwa kwa msaada wa Serikali ya Norway na nitangaze tu kwamba wageni wote hao, kwenye ukumbi wa Pius Msekwa, watakutana na Kamati ya Mambo ya Nje, karibuni sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Chegeni kwa kuwa na Mradi kama huu wa Haki na Demokrasia pengine Majimbo mengine yangependa kuchota kwake ili kuona ushirikiano kama huu unasambaa katika Majimbo mengine. *(Makofi)*

Tunao vijana kumi na tano kutoka Taasisi ya Vijana *(TAYOA)*, wakiongozwa na Mkurugenzi wa *TAYOA*, Ndugu Peter Masika, karibuni sana. Mara kwa mara tunawaona mkija kuangalia shughuli hizi, karibuni sana ni haki zenu.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa William Ngeleja, ambaye anaitwa Fred Andrew Lukeki, anatoka Jimboni kule Sengerema, yule pale karibu sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Fatuma Maghimbi, ambao ni ndugu Ipyana Tumaini Mwakifyange na mwenzie Suna Zuberi Ngajima. Hakusema wanatoka wapi lakini Tanzania hii ni kubwa nadhani wanahusiana, karibuni sana.

Mheshimiwa Masolwa, Mbunge wa Bububu, anao wageni kutoka Jimbo la Bububu ambao ni Mwenyekiti wa Jimbo, Katibu wa Jimbo, Katibu Mwenezi na Wenyeviti wawili wa *Ward* na Wenyeviti wa Matawi watano kutoka mjini Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa matangazo mengine, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, ameniomba nitangaze kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati ya Mambo ya Nje, saa tano asubuhi hii ya leo, ukumbi namba 231.

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anaomba Wabunge wote ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwamba mara baada ya kipindi hiki cha asubuhi cha maswali na majibu, wakutane ghorofa ya nne, ukumbi Na. 428.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, anawataka wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, wakutane saa tano asubuhi ukumbi Na. 133.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakutane leo saa kumi jioni katika ukumbi 219, ghorofa ya pili, jengo la utawala.

Mheshimiwa George Malima Lubeleja, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo pamoja na wajumbe ya Kamati ya Huduma za Jamii, hiki ni kikao cha pamoja, wakutane leo saa saba mchana kwa ajili ya kukutana na wananchi wenye ulemavu. Wananchi wenye ulemavu wamekuja hapa Bungeni wanataka kuonana na Kamati hizo mbili, itakuwa saa saba mchana.

Mheshimiwa Khatib, Katibu Msaidizi wa Wabunge wa CCM, anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ya *CCM Caucus*, wakutane saa tano kwenye ukumbi wa Spika ghorofa ya kwanza. Hiyo nadhani ndiyo itafuatiwa na Mkutano wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, saa saba na nusu. Hapa ndiyo mwisho wa matangazo.

Namuomba sasa Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti, kwa sababu nina mikutano mingine, aje kushika Kiti na kuendelea na shughuli nyingine.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## KAULI YA WAZIRI

### TAARIFA KUHUSU WAGONJWA WAWILI WALIOFANYIWA UPASUAJI TOFAUTI NA MATATIZO YAO KATIKA TAASISI YA MOI

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa kauli ya Serikali. Kabla sijafanya hivyo, ningependa nitoe shukrani nyingi sana kwa wana CCM wenzangu, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wajumbe wa Mkutano Mkuu, kwa heshima waliyonipa mimi na Naibu Waziri wangu na kututeua kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku za hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa kuhusu wagonjwa wa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili yaani MOI ambao walifanyiwa upasuaji tofauti na matatizo yaliyokuwa yanawasumbua. Tukio hili, lilitokea tarehe 1 Novemba, 2007 ambapo mgonjwa Emmanuel Didas mwenye umri wa miaka 20 aliyekuwa na tatizo la goti la kushoto alifanyiwa kwa makosa upasuaji wa kichwa ambapo Emmanuel Mgaya mwenye umri wa miaka 19 mwenye tatizo la kichwa alipasuliwa goti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya pili, tarehe 2 Novemba, 2007, Bodi ya Wadhamini ya Taasisi ya Mifupa, ilikutana na kuunda Tume ya Kuchunguza chanzo cha mkanganyiko uliojitokeza. Tume hiyo ilipewa hadi Jumanne tarehe 13 Novemba, 2007, kukamilisha uchunguzi wao na kukabidhi ripoti tarehe hiyo au siku kabla. Aidha, Bodi iliwasimamisha kazi Madaktari wawili waliohusika na upasuaji na kuagiza watumishi wote waliohusika na matayarisho ya wagonjwa kabla ya kupelekwa chumba cha upasuaji waandike maelezo kuhusu jinsi walivyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaomba wananchi wasubiri Taarifa ya Tume na inatoa rai kwa wananchi na vyombo vya habari kwamba jambo hili ni nzito sana na nyeti kwa hiyo ni muhimu lizungumzwe bila kupotoshwa kwani upotoshwaji unaweza kujenga hofu isiyo ya kawaida kwa wananchi. Ukiacha kutokea kwa tukio hili, huduma za Taasisi ya MOI zinaendelea kama kawaida, Serikali inawaomba wananchi waendelee kuwa na imani na taasisi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa taarifa kwamba mgonjwa aliyepasuliwa goti, kidonda chake kimepona ambapo yule aliyepasuliwa kichwa amezinduka kutoka hali aliyokuwa nayo ya kutojitambua, hajaanza kuongea lakini anawasiliana na Wauguzi kwa ishara. Baada ya kupokea ripoti ya Tume ya Uchunguzi, Wizara yangu itaipitia taarifa hiyo kwa makini na kuchambua masuala ya kitaalamu na kimaadili yatakayojitokeza na kuziagiza Bodi za Kitaaluma kutoa maoni yao Serikalini katika muda mfupi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali imesikitishwa sana na kutokea kwa mkanganyiko huu na inatoa pole kwa wagonjwa, ndugu zao na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## HOJA ZA WABUNGE

## TAARIFA YA BENKI YA RASILIMALI YA TANZANIA YA MWAKA 2006

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha hoja yangu ambayo ilijengeka wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Fedha anawasilisha Mezani Taarifa ya Benki ya Rasilimali Tanzania (*TID*) ya mwaka 2006, nilitoa hoja kwamba Bunge lako lipewe fursa kujadili taarifa hiyo na hoja hiyo ilikubaliwa. Taarifa hiyo iliwasilishwa katika Mkutano wa Nane uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo umepanga hoja hii katika shughuli za Bunge za leo, kwa hiyo, natoa maelezo yafuatayo ili Wabunge wenzangu waweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha ya hoja yangu, ni kutaka kuangalia namna ambayo Benki hiyo inahudumia sekta ya kilimo ambayo ina umuhimu mkubwa na hatimaye kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda wa miaka minne kuanzia mwaka 2003/2006 Benki ya Rasilimali (*TID*) imetoa mikopo kwa ajili ya kilimo kama ifuatavyo:-

Mwaka 2003, ilitoa mikopo miwili ya kilimo yenye thamani shilingi milioni 766,500,000, mwaka 2004 Benki hiyo ilitoa mikopo minne ya kilimo yenye jumla ya shilingi bilioni 6,569,000,000 na katika mwaka 2005, Benki hiyo ilitoa mikopo sita yenye jumla ya thamani ya bilioni 4,039,500,000. Mwaka 2006 ilitoa mikopo mitano kwa miradi mitano yenye jumla ya shilingi bilioni 5,940,284,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijumulisha miradi hii ya kilimo katika miaka hii minne, (*TID*) imetoa mikopo kwa miradi ya kilimo 17 ambayo ina thamani ya shilingi bilioni 17,315,284,000. Ukiangalia miradi hii utaona kwamba fedha nyingi hapa zimekwenda kwenye makampuni. Kwa upande wa kilimo zaidi zimekwenda kwenye wakulima wakubwa wa maua. Vile vile kwenye kampuni ya sukari ya Mtibwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia taarifa ya *TID*, nimeona kwamba katika miaka hii minne 2003 mpaka 2006, wametoa mikopo kwa makampuni/miradi 186.

Katika miradi hiyo, miradi ya kilimo kama nilivyokwishaeleza ni 17. Kwa hiyo, katika miradi yote ambayo imepewa mikopo, mikopo ya kilimo na usindikaji ni sawa sawa na asilimia 20.98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii, inaonekana waziwazi kwamba maendeleo ya kilimo hayawezi kupatikana kwa kutumia masharti ya mikopo yaliyopo. Vilivyo Benki zilizopo hapa nchini hazina masharti yanayozingatia muda wa kuanza mradi wa kilimo hadi kuanza kuvuna. Kwa mfano, katika zao la chai kutoka kupanda hadi kuvuna inachukua miaka mitatu hadi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tutazame kidogo mazao mengine. Mkonge unachukua miaka mitatu, korosho miaka 6, kahawa miaka 4, mpira miaka 6 mpaka 7, michungwa miaka mitatu hadi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda huu wa kupanda hadi kuvuna haujumlishi muda wa kuandaa vipando/miche. Nikiwa na maana kwamba ni muda zaidi kuanzia kutayarisha miche mpaka wakati wa kupanda. Kwa mfano, kwenye zao hili la chai ambalo mimi nalielewa maana ni mkulima wa chai, vipando, hapa tunatumia neno vipando kwa sababu kuna chai inaitwa *Cronal Tea* ambayo siyo miche lakini ni vitu ambavyo unafanya kwa Kingereza tunasema *barding* inachukua miezi 12 kuandaa bustani. Sasa ukichukua na ile miaka mitatu mpaka minne, ni takribani miaka mitano bado hujaanza kupata mazao ili uweze kulipa mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kusema kwamba shabaha ya kutoa hoja wakati Waziri wa Fedha anawasilisha Mezani Taarifa ya Benki ya Rasilimali kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge, kuwa Bunge lijadili taarifa hii ni kutaka kuwapa Wabunge fursa ya kujadili suala la mikopo ya kilimo kwa kina na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo sasa ni kwamba bila kuwepo utaratibu wa mikopo unaozingatia muda wa miradi ya kilimo inaochukua hadi mazao kuvunwa basi ni wakulima wakubwa tu ndiyo wanaweza kukopeshwa au kukopesheka maana wanavyo vyanzo vingine vya kuweza kulipa mikopo hiyo hata kabla ya kuanza kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kuwa idadi kubwa ya Watanzania takribani asilimia 80 huishi vijijini na hutegemea kilimo basi azma ya kuondoa umaskini kwa kupitia kilimo itabaki kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi napendekeza kwa Bunge lako Tukufu kwamba sasa lijadili Taarifa ya Benki ya Rasilimali Tanzania na kuishauri Serikali kuandaa utaratibu mahususi utakaowawezesha wakulima wadogo kukopa na kuendeleza kilimo. Utaratibu huo uwe ni pamoja na kufikiria kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(Agricultural Development Bank)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa William Shellukindo, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema mwanzo kwamba Kanuni zetu za Bunge zinaruhusu Mbunge mmoja mmoja kuleta hoja kwa nia ya kujadiliwa na Bunge kwa lengo mahususi na Mheshimiwa Shellukindo ametumia fursa hiyo kwa kuleta hoja hii mbele yenu ambayo amependekeza kuwa Bunge lijadili taarifa ile ambayo iliwasilishwa Mezani wakati ule inayohusiana na Benki ya Rasilimali Tanzania kwa ni ya kuishauri Serikali kuandaa utaratibu mahususi utakaowezesha wakulima hasa wakulima wadogo kukopa na kuendeleza kilimo, utaratibu huo uwe ni pamoja na kufikiria kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*Agricultural Development Bank*). Kwa hiyo, hilo ndio pendekezo lake na ndio kitu ambacho kipo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo tunayo nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii iliyotolewa na mwenzetu Mheshimiwa William Shellukindo (*Senator)* na ninao wachangiaji kwa kuanzia watatu lakini kama yupo Mheshimiwa Mbunge mwingine yeyote angependa kushiriki katika mjadala, tafadhali anaruhusiwa aniletee kwa maandishi. Kwa hiyo, moja kwa moja, sasa ninawaita wachangiaji, hii ni moja kwa moja haina kuwaita Kamati au Upinzani hapana, ni uchangiaji wa moja kwa moja ,kwa hiyo wa kwanza kabisa atakuwa ni Mheshimwa George Simbachawene Mbunge wa Kibakwe.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kutoa mchango katika hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa William Shellukindo inayohusiana na maendeleo ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kufanya hivyo, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kutoa salamu zangu za rambirambi na pole kwa msiba uliotukuta wa marehemu Salome Mbatia. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja ya Mheshimiwa William Shellukindo, ni hoja ambayo kwa kweli inahusu uhai wa Taifa. Tumekiri katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwamba kilimo ndio njia pekee inayoweza kutukomboa tukaachana na umaskini lakini binafsi ninavyoona namna ambavyo tunashughulikia mipango ya kilimo sambamba na mipango yote ya MKUKUTA, MKURABITA na mambo mengine, kwa kweli kwa hakika hatuwezi tukafikia lengo kama hatutakuwa na mipango mahususi na hasa ya namna ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wakulima wanaogawanyika kwa takriban makundi matatu. Tunao wakulima wadogo, tunao wakulima wa kati na wakulima wakubwa na tunayo mazao yanayogawanyika hivyo hivyo, tunayo mazao yanayolimwa kwa muda mfupi, tunayo mazao yanayolimwa kwa muda wa kati mwaka mmoja hadi miwili au mitatu lakini pia tunao wakulima wanaolima mazao ya kipindi kirefu kama korosho na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiisoma Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010, tumeeleza katika Ibara ya 30, Sura ya Tatu, kipengele cha (I), kinasema kwamba:-

"CCM itaona kwamba Serikali inahimiza na kushauri juu ya umuhimu wa mazao ya kudumu kama minazi, michungwa, miembe, mifenesi, mikorosho, mibuni, michai, michikichi na kadhalika"

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Ibara hiyo hiyo, kipengele cha (L), naomba kwa ruhusa yako ninukuu:-

"CCM itazitaka Serikali kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo inatengewa si chini ya asilimia 10 ya uwekezaji unaofanywa na Serikali sambamba na malengo ya *SADC"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma tu hivi, nadhani unapata msukumo kwamba Serikali inapaswa kufanya mambo muhimu yafuatayo pamoja na mipango mikubwa kama ya *DADP's* ambayo inafanya vizuri lakini katika *level* ya majaribio na utafiti na kwamba bado haijaingia kwenye kilimo chenyewe. Kwa hakika, kama tukitegemea tu mipango kama hiyo peke yake, hatuwezi tukafika mahali popote. Jambo kubwa hapa ni namna gani tutamsaidia mkulima. Namna gani tutamfanya mkulima huyu aweze kuingia kwenye kilimo hicho cha kisasa, kuzungumza tu bila ya kufikiria namna ya kumsaidia, kumfundisha kwa kumfanya awe na vitalu, hakuwezi kukamsaidia, haionyeshi hapa kwamba Serikali ipo *serious* kiasi gani katika kumsaidia mkulima huyo. Kwa mfano wengi tulidhani kwamba mkulima huyu mdogo kabisa wa chini ambaye shida yake ni *power tiller* siyo hayo mabilioni mnayotaka, shida yake ni *power tiller* tu na *power tiller* ni karibu milioni tano tu, tukaamini kwamba kwa Mpango wa Mfuko wa Pembejeo ambao upo huyu mtu angeweza kutoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie hadi sasa utekelezaji wa hilo haujafahamika kwa wengi au hauko wazi kiasi cha kwenda kwenye malengo ya *performance.* Mfuko wa Pembejeo upo lakini sijui unamsaidia nani na kwa kiasi gani, una fedha kidogo au ni urasimu tu wa kuwasaidia watu, hasa wakulima wanaoishi vijijini? Hii ni kasoro kubwa na hatuwezi tukafikia lengo lililotajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja katika suala la mabenki, mabenki yaliyo mengi sasa hivi ni mabenki ya kibiashara, mabenki yanayo-*deal* na makampuni yanayo-*pack* bidhaa, ni mabenki yanayo-*deal* na viwanda lakini hakuna benki mahususi katika nchi yetu inayoshughulika na mkulima, kwamba hii ni benki maalum ya kushughulika na

mkulima. Tunazo benki nyingi tu na zina mitaji mikubwa baada ya wawekezaji kuingia nchini lakini benki hizo hazina urafiki na mkulima na kwa tafsiri ya moja kwa moja Tanzania mkulima ndio mtu maskini. Kwa hiyo, tunasema mkulima ni mtu muhimu lakini mkulima wa Tanzania ndiye maskini. Kama hakuna mpango maalum kwa ajili ya kumsaidia huyu mkulima kwa hakika ni kwamba hatuwezi tukafikia lengo la *millenium* na wala hatuwezi tukafikia malengo ya MKUKUTA na wala hatuwezi tukafikia malengo ya Ilani yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote haya mabenki ya biashara, hakuna siku yeyote Duniani mabenki ya kibiashara yamewahi kuwa na urafiki na mtu maskini na kwa tafsiri niliyoisema ni kwamba Tanzania mkulima ndiye maskini, ndiye anayeishi kwenye nyumba mbovu, mkulima wa Tanzania ndiye anayetembea umbali mrefu kuliko hata msanii anayeishi Dar es Salaam, mkulima wa Tanzania ndiye anayekula chakula ambacho hakipo katika viwango na kwa maana hiyo tunapata tafsiri halisi ya kwamba huyu ndiye mtu maskini. Lakini huyu mtu ana ardhi, huyu mtu anayo nguvu, huyu mtu tunasema tunapeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri watu wapewe elimu na wanapewa elimu kwa kiwango fulani, lakini bila kumtafutia mtaji, hawezi akatoka pale alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hakuna benki Tanzania maalum kabisa kwa ajili ya kumsaidia mkulima. Nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa William Shellukindo kwa asilimia mia kwa mia na kama nimemuelewa vizuri, Mheshimiwa William Shellukindo kwa sababu hoja yake ilitokana na taarifa ya *TIB* ambayo kwa miaka hiyo yote karibu mitano, sita hivi imetoa mikopo 17 tu kwa wakulima na fedha yenyewe nadhani ni kidogo kuliko iliyoenda kwenye madini, kuliko iliyoenda kwenye biashara. Ninaamini Mheshimiwa William Shellukindo ameleta kitu chema na nafikiria kwamba siku ya leo kwa kweli Serikali ni vizuri ikaliona hili dai la kwamba kuwepo na benki maalum kabisa kwa ajili ya kushughulikia na wakulima wadogo, wa kati na wakubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na fikra ambayo tulikuwa tumedhani sisi tunaokaa vijijini, tukaamini itakuja kutukomboa sisi wenye shida ya kuwa na jembe la plau, wenye shida ya ng’ombe wa kulima ambaye anahitaji pengine mtaji wa Sh.500,000/= tu aweze kuwa na zana za kufanyia kazi badala ya kufanya shughuli za shulubu kwamba hii mikopo inayoitwa mikopo ya Mheshimiwa Rais JK ambapo kila Mkoa ulipewa shilingi bilioni moja tukadhani pengine inaweza ika-*come up* na *solution* ya wakulima hawa wadogo wadogo maana wangepata fursa ya kuweza kuchukua hiyo mikopo midogo midogo. Lakini mambo siyo hivyo. Nasema tunashukuru tu kwamba hela hizo zimetoka na baadhi wamenufaika lakini mimi binafsi kwa mfano nikichukulia Jimbo langu la Kibakwe, sina taarifa kama kuna mtu hata mmoja aliyepata mkopo awe mfanyabiashara au mkulima na mkulima ndiyo kabisa hakuhesabika katika mgao wa mkopo ule. Kwa hiyo, wakulima hapa napo hawakuweza kuheshimika na kufikiriwa na mabenki yale yamekataa kuwakopesha wakulima na kama yamefanya hivyo basi nadhani ni sehemu nyingine na pengine ni kwa kiwango kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tu tunarudi pale pale kwamba kwa kweli mkulima wa Tanzania ameshindwa kupata chombo cha kumsaidia. Serikali ione haja sasa ya kuanzisha benki maalum kwa ajili ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ili waweze kukopa kuliko sasa ambavyo wakulima wanahangaika, hawajui hata wanaweza wakasaidiwa kwa chombo gani, kila mahali wanakataliwa. Ukienda *CRDB* wanakwambia kilimo sisi hatuna *guarantee* nacho, ukienda *NMB* hali kadhalika, ukienda Mfuko wa Pembejeo unakutana na urasimu. Kuna *DC* mmoja anaitwa Kasege amestaafu akiwa yupo Bagamoyo pale, akiwa *DC* amefanya *follow up* ya mkopo wa trekta na ana mashamba mazuri na yana Hati Miliki nzuri lakini mpaka leo hajawahi kupata mkopo. Mkopo unatolewa na benki iliyopo Dar es Salaam, *Barclays* inapewa jukumu la kukopesha Mfuko wa Wakulima, *Barclays Bank* yenyewe haipo hata Wilayani, kwe kweli nashindwa kuielewa, Serikali *has to be serious* na jambo hili kwa kweli tusiishie kusema maneno tu tufanye vitu ambavyo vinatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na hoja hii ya Mheshimiwa William Shellukindo na nimpongeze binafsi kwa kuleta hoja hii. Kwa kweli nia yake na sababu na umuhimu wa hoja hii ni mkubwa kuliko pengine tunavyofikiria kwa maana ya hali halisi ya nchi yetu na namna tunavyoweza kuwakomboa watu wetu katika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niwezi kuchangia kidogo juu ya hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba pia kwa niaba ya wananchi wa Masasi, nitoe rasmi rambirambi zangu kwa kifo kilichotupata cha kufiwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Wanawake, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Salome Mbatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, naomba nitoe pongezi za dhati kwa viongozi wote waliochaguliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa CCM hasa hasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wengine wote waliofuata. Kwa kweli uchaguzi ule ulionyesha demokrasia ilivyokomaa katika Chama chetu cha CCM na ninaomba wenzetu wa Vyama vya Upinzani wafuate mfano huo sio kuchaguana tu ila mradi wapo katika sehemu zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa William Shellukindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wakati mwingine ni lazima tuseme kwamba haya mambo tunajitakia sisi wenyewe. Ukiangalia historia yetu toka tupate uhuru mpaka leo hatujawa *very serious* katika suala la kilimo na hasa katika kutafuta nyenzo za jinsi gani kilimo hiki tutakikuza katika nchi yetu. Ni kweli tumekuwa na mabenki, tulikuwa na Benki ya Maendeleo ya Nyumba *(THB)* na hii ya *TIB*, ni benki za zamani kidogo lakini ukiangalia *THB* ilikufa kifo cha mende na ilikufa kwa sababu ilikuwa inasaidia zaidi watu maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nilikuwa naitembelea Benki ya *THB*, kila ukienda unakuta watu wengi, wa kawaida tu, mle ndani hakuna hata mtu mmoja ambaye amevaa suti, nikajiuliza hii kweli ni benki? Kweli haikuchukua muda ilikuja kufa kwa sababu zaidi ilikuwa inahudumia makabwela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki hii ya *TIB* nayo ni ya siku nyingi kidogo ambayo ilijikita zaidi kukopesha matajiri na kuendelea na imefanya vizuri katika sehemu mbalimbali lakini haikuweza kumkomboa Mtanzania katika kuhakikisha kwamba anapata manufaa yoyote yale katika shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoona ripoti hii na kuisoma kidogo, nimeona kwamba wakati umefika wa Serikali kuangalia masuala haya na kuamua tunaweza kufanya nini ili kuwasaidia hawa Watanzania wetu. *TIB* ndiyo benki peke yake tunayoweza kuitegemea siyo tu katika kuendeleza viwanda lakini hasa katika mambo haya ya kilimo na kama Mheshimiwa William Shellukindo alivyosema, msaada sasa hivi unaenda zaidi katika kilimo kikubwa kwa mfano huko Mtibwa, Kagera, maua na kadhalika, ni kilimo cha watu wakubwa si kilimo cha wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa huko kwetu Kusini sasa hivi kunafunguka upesi sana na nimewahi kusema katika Bunge hili kwamba maeneo ya Kusini yana ardhi kubwa sana ambayo haitumiki. Maeneo ya Rufiji mpaka Matandu mpaka Mbwenkuru unafika maeneo ya Lukuledi, haya yote ni maeneo makubwa na mazuri lakini ni mapori. Ukienda tu kuangalia lile pori kubwa utaona kama vile linakuuliza, bwana kuna nini unachokita hapa? Kwa kweli bila kuwa na *D6* lile linaloweza kuangusha miti, huwezi ukaliingia pori lile kwa kutumia jembe la mkono. Maeneo haya yote hayawezi kutumiwa bila kuwa na vyombo vikubwa kama magreda ya *D6*, matrekta na vifaa vingine. Maeneo haya yanaweza kuwa maghala makubwa ya uhakika wa nafaka nchini. *TIB* ndio inaweza kuwa mkombozi wa kuibua kilimo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita mimi mwenyewe binafsi nilitembelea Benki ya *TIB* pale Makao Makuu. Nia yangu ilikuwa kwenda kujua endapo mtu unaweza kukopa kwa mfano *D6* ili ikapambane na misitu ya kule kwetu. Wataalam wakaniambia, mzee karibu sana lakini ili uweze kuendelea unahitaji uandike *business plan*. Sasa nikasema *business plan* nitaiandika namna gani, si kazi yake benki yenyewe ndiyo iwe na wataalam wa kutosha watakaokuwa na uwezo wa kuandika hizo *business plan* halafu itupatie wateja? Tukipata *business plan* nzuri, tunaweza kurudisha gharama. Wao walisema kwamba kwa upande wa kilimo, shida kubwa kwa benki ni ule uhakika je, mambo yakienda kombo fedha zao zitarudi namna gani? Ndiyo wakaniambia, kwa kweli mpaka sasa kwa taratibu zao wanatumia Hatimiliki za nyumba na masharti ya Hatimiliki za Ardhi, sio rahisi kwa wakulima wote. Kwa hiyo, niliona wenzetu hawapo katika maandalizi ya sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinieleza pia kwamba hata Serikali ilikuwa inafikiria kuwekeza karibu shilingi bilioni 50 katika benki ya *TIB* ili wananchi waweze kukopa lakini hata hivyo mpaka leo hakuna chochote kilichofanyika. Kwa hiyo, nataka kusema

haya mambo si kwamba hayawezekani, inawezekana ikiwa tutaamua kwamba sasa hivi tufanye utaratibu wa makusudi wa kuhakikisha tunakuwa na Benki ya wakulima. Endapo kilimo hatutakivalia njuga na hasa kukivalia njuga kupitia mikopo ya mabenki basi, umaskini Tanzania utaendelea kutunyemelea na itakuwa vigumu sana kuutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kupitia uchokozi, uchokozi kama huu wa Mheshimiwa William Shellukindo, hebu tujadiliane taarifa juu ya benki hii. Nafikiri kama tukiiunga mkono na Serikali ikae na wataalam wake kuona jinsi gani wanavyoweza kupeleka rasilimali fedha zaidi kwa benki kama hii, nafikiri kwamba inawezekana tukayaondoa haya. Masharti ya mkopo ni magumu lakini nafikiri Watanzania wako tayari kutimiza masharti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kurudia kuunga mkono hoja hii na tunaiomba Serikali iingie ndani zaidi katika kushughulikia suala hili ili tuweze kuwa na MKUKUTA utakaotokana na benki kama hizi, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ADAM K. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniweka na mimi kwenye orodha ya wachangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwa dhati kabisa, nimshukuru Mheshimiwa William Shellukindo kwa kuileta hoja hii kwa sababu nadhani katika kipindi changu nilichokuwa Bungeni, ndiyo mara ya kwanza tunajadili hoja ya Wabunge, nimeiona tu katika Mabunge mengine. Hili ni jambo kusema kweli ambalo wewe kama mzee wa kanuni utakubaliana na mimi kwamba ni sehemu mojawapo nzuri ya matumizi ya haki zetu kama Wabunge ya kuhoji mambo mbalimbali. Kwa hiyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa William Shellukindo kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu na mimi pia ni mara yangu ya kwanza ninasimama humu ndani, naomba nitoe rambirambi zangu kwa familia ya Mheshimiwa Salome Mbatia. Kwa bahati nzuri, nilikuwa naye siku mbili kabla ya kwenda kwenye ziara yake Kigoma na kule tulikutana na kusema kweli matarajio yake kwa nchi hii na kwa Bunge hili na kwa utekelezaji wa majukumu yake kama *NEC*, tumempoteza mwenzetu ambaye alikuwa na malengo makubwa sana. Mungu amjalie huko kwenye safari yake mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii pia nimwombee nafuu ya haraka ndugu yangu Mudhihir, Mungu amjalie afya njema aweze ku-*recover* haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye shughuli hii, Mheshimiwa William Shellukindo amezungumzia mikopo kwenye kilimo na alikuwa anazungumzia *TIB,* kwa bahati nzuri ninaifahamu vizuri na alikuwa anajaribu kuzungumzia umuhimu wa mikopo ambayo inatolewa na *TIB* na sura yote ile ya utoaji wa mikopo kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka yoyote kama tusipofanyia haraka kutafuta ufumbuzi wa tatizo hil,i tatizo litakuwa kubwa zaidi na kwa kweli tutakuwa

tunazungumzia masuala ya MKUKUTA na nini lakini tutakuwa tunapiga hatua mbazo tutakuwa tunazunguka hapo hapo hatuendi mbele. Kwa sababu kwa takwimu tu kama tunavyokubaliana sisi wote humu ndani asilimia 80 ya Watanzania wako kwenye maeneo ya kilimo hata kama wakiwa mijini lakini kwa namna yoteyote ile watakuwa na mahusiano fulani na sekta ya kilimo.

Sasa benki zote zilivyo sasa hivi, *NBC*, *CRDB*, *STANDARD CHARTED* zinatengeneza faida kubwa sana hivi zilivyo leo bila kuingia kwenye kilimo. Kwa hiyo, kimsingi hawana *motivation* ya aina yoyote ya kwenda kwenye kilimo.

Sasa basi, kwa kuwa hii ndiyo benki ambayo 99% inamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ni haya mambo ambayo tunayazungumzia ni lazima tuyaelekeze *TIB*. Hatari ya kutokufanya maamuzi ya haraka ya kuiwezesha *TIB* au benki yenye uwezo ni kwamba sekta ya kilimo itaendelea kudumaa kwa sababu hakuna mtu mwingine atakayekwenda kuweka pesa benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hoja zinazozungumzia za kutokupeleka pesa kwenye kilimo ni hoja za msingi ama ni *economic science* mtu anakwambia kuna masuala ya *risk, collateral, capitalisation, technological disadvantages* kwenye kilimo bado watu wanalima kwa mkono utakwenda vipi kumwekea shilingi milioni 20 au milioni 30? Katika lugha ya kibenki yote yatakubalika lakini kuna suala la uhakika kabisa la maisha ya Watanzania. Kwa hiyo, *whatever economic science* inavyosema ni lazima humu ndani tukae na tutafute ufumbuzi wa namna ya kuwapatia wakulima wadogowadogo, *otherwise* wataendelea kudumaa hapo hapo. Kwa hiyo, hakuna mtu mwingine ambaye tunaweza tukampa suala hili au tukaizungumzie Serikali kuiomba itusaidie zaidi ya *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna kitengo tulikiona katika hotuba ya Waziri Mkuu cha *Rural Finance Unity*, nadhani kipo *somewhere* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini mimi nilikuwa nimeomba kwamba labda kitengo hicho pia kiangaliwe namna kinavyoweza kufanya kazi na TIB na mashirika mengine na idara nyingine husika ili kuangalia uwezekano wa kuyaondolea matatizo yote yale ambayo yanaikwaza *TIB* kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya matatizo hayo ni *capitalisation*. Kwa muda wa miaka mitatu sasa Wizara ya Fedha inajua kwani kila wakija kwenye Kamati ya Fedha wanatuambia kwamba kuna tatizo la *capitalisation* na *TIB* wenyewe wanasema. Kama wakiweza kufikia *capital* au mtaji wa shilingi bilioni 50 pesa za Tanzania wanakopesheka wao wenyewe kwa fedha za mashirika mengine makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi Shirika la *TIB* wana mtaji wa shilingi bilioni 16 au 17 wakati mashirika kama haya ya nchi nyingine yana mtaji wa shilingi bilioni 500. Kwa hiyo, utaona kwamba hili Shirika lipo lakini uwezo wake wa kukidhi mahitaji ya Watanzania kusema kweli ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wameyasema mambo na mimi nataka nizungumzie suala lingine. Naomba tukubaliane kupitia hoja hii ya Mheshimiwa William H. Shellukindo kwamba kuna mashirika Tanzania ambayo yana fedha ambayo yanamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naomba niyazungumzie mashirika manne yaani *PSPF, NSSF, PPF* na *BoT* yaani Benki Kuu ya Tanzania. Kila mmoja akitoa dola milioni 500 na Benki Kuu kwenye akiba yake ikatoa dola milioni 10. Tuna-*capitalise TIB* kwa shilingi bilioni 30, tunawapa uwezo wao wa kuzunguka na kutafuta fedha za ziada ili waje kuwakopesha wakulima kwa uwezo wa shilingi bilioni 60 au 70. Sasa hapo tutaanza kuzungumzia sijui tunasema, "Sheria hii unajua labda Sheria ya Benki Kuu hairuhusu kukopesha lakini Sheria zenyewe zinatungwa humu ndani ziletwe na tuzibadilishe!" Lakini tusijikwaze kwa yale ambayo tunajiwekea wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani nimesoma katika Taarifa hii kama ilivyoletwa. Ukiisoma kuna mambo mazuri mazuri tu yanasemwa humu lakini kama utekelezaji wake haukidhi haja ya Watanzania walio wengi ukopeshaji benki hutoa huduma za kifedha nchini Tanzania kwa utaratibu ufuatao: kutoa au kushiriki katika mikopo kutoka kwenye mtaji wake; kutoa fedha zilizotajwa katika vifungu; kudhamini mikopo yenye lengo la kuendeleza uchumi lakini mkulima hayumo humu. Yumo humu kwa malengo ya maneno lakini yule mkulima wa kule kwetu Mkuranga, karibu Mwenyekiti siku ukipata nafasi ya kuja.

Kule kwetu Mkuranga tuna zao la Korosho, nimelisema humu wakati wa Wizara ya Kilimo na wakati wa Wizara ya Fedha. Zao la Korosho nchi nzima likipatiwa shilingi bilioni 6 mpaka 7 kwa kilimo cha kuanzia Tanga mpaka Mtwara. Mzee William H. Shellukindo amesema zao kupanda mpaka kupata ni miezi sita, si kweli kwani mbegu mpya sasa hivi ni miaka mitatu mpaka mine. Nakuhakikishia kwa sayansi kabisa kwamba kama tukipata shilingi bilioni 7 kwenye zao la korosho, baada ya miaka minne tutachangia shilingi bilioni 40 kwa uchumi wa nchi hii na tunalisema tukalisemee wapi? Lazima kama Mzee William H. Shellukindo alivyolileta tulisemee kwenye Serikali ili wao kama Serikali watafute namna ama kupitia *TIB* au Bodi za Mazao lakini tutafute namna ambayo sasa *Rural Financing* isikwazwe na matatizo ya *economic theory*. Sisi hatuna uwezo wa kukaa na kujadiliana *what is right and what is wrong, what is right* ni kwamba lazima mkulima mtanzania apatiwe namna ya kuwezeshwa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili pia ni lazima tuwe waangalifu kidogo kwa sababu kuna tofauti baina ya uwezeshaji na nimelitafuta neno nimelikosa. Kwa hiyo, nimeliita *UMITAJIZISHAJI*, ndiyo nimelitafutia neno hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuwawezesha mitaji wakulima kama ninavyosema si suala la *option* na iende sambamba na elimu kwamba ukipewa shilingi milioni 2 au 3 basi unatarajiwa uwe umezalisha shilingi milioni 3 au 4 ili zirudi ziwe *sustainable* au ziwe endelevu na watu wenye kufanya hii ni *TIB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema mtoa hoja kuna shilingi bilioni 42 za usimamizi wa fedha za mifuko, hizi ni *Government Guarantees* zinatoka *BoT*, ni benki zetu sisi wenyewe. Lakini pesa hizi zinatolewa kwa wenye uwezo wale ambao wanaweza kuandika *right up* nzuri na kwenda kuchukua shilingi bilioni 5 au 6, ndiyo watu wa mboga mboga, watu wa maua na kadhalika. Lakini lazima tutafute ufumbuzi kwamba *somewhere somehow* watu wale wadogo wadogo au hata kama kuna miradi ya mtu *capital* kubwa kwenda kuchukua shilingi bilioni 5 ni lazima iwe na *public private initiatives* ambazo zinahakikisha kwamba hii miradi inayodhaminiwa na pesa za Serikali lazima iwe ina *guarantee participation* ya wakulima wadogowadogo. Kwa sababu kwa njia hiyo ndiyo tutapata *technological transfer*, ndiyo tutapata ujuzi na ndiyo tutapata *employment generation* kwa hawa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niungane na yote yaliyosemwa na Mheshimiwa George B. Simbachawene na Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope. Lakini naomba nisisitize kwamba kama tuna uwezo Serikali izingatie *capitalisation* kuwaongezea fedha *TIB* kutoka kwenye hii mifuko ambayo ina pesa nyingi tu ili *TIB* kwa makusudi kabisa na hapa samahani naomba nimalize; hapa kuna suala la urekebishaji wa *TIB*. Sasa wanasema muundo wa huduma zitakazotolewa na *TIB* baada ya urekebishaji utazingatia mahitaji ya mikopo ya kibiashara pamoja na mikopo, *no!* iwe *specific* kama tunakujazeni hela iwe *specific* kwamba tunataka mikopo yenu pamoja na kuwa na *balance act* ya watu wakubwa wakubwa izingatie namna ya kuwanufaisha wakulima wadogowadogo, iwe ni *specific*. Sasa isiwe ni kitu ambacho ni *vague* tu, juujuu. Na bila kufanya hivyo ninaomba nirudie tena siioni mimi *NMB* au *CRDB* ya hivi sasa wakienda kutoa mikopo kwa wakulima wadogowadogo wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme wazi kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa William H. Shellukindo na naiomba Serikali itusaidie kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Ahsante sana tunakushukuru sana Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima. Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Lucy Sawere Nkya. Profesa Karibu!

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ili nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ambayo naiona ni ya msingi na inaletwa wakati muafaka na kwa kweli ninapochangia napenda niseme nachangia kwa nia nzuri sana na kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Ludewa kutokana na haya nitakayoyasema. Mimi siyo mtaalamu wa uchumi lakini nataka nionyeshe jinsi ninavyopenda kuthamini hoja inayoletwa ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili kujiletea maendeleo yao wenyewe lakini vilevile kuchangia kwenye pato la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kusema kwamba kama ingekuwa inawezekana kuwa na asilimia zaidi ya mia basi mimi hapo ningeweza kusema nakubaliana na hoja hii kwa zaidi ya asilimia mia moja ili kutoa uzito wa hoja yenyewe.

Napenda nitolee mifano mizuri tu ya Ludewa ili kuonyesha jinsi ambavyo wananchi wa Wilaya ya Ludewa wanaweza kufaidika sana kutokana na kuwa na utaratibu wa benki kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa kwanza nimewahi kuzungumza hapa nadhani siku mbili zilizopita kwamba katika Wilaya ya Ludewa sote tunajua kwamba kuna miradi ya chuma cha Liganga pamoja na makaa ya mawe. Na hapa tumesikia tena Mheshimiwa Waziri wa Madini na Nishati akizungumzia. Ninajua kwamba kuna mipango kabambe ya kuhakikisha kwamba miradi ile ya chuma cha Liganga na Mchuchuma inaanza katika kipindi hiki yaani kabla ya 2010.

Lakini vilevile kuna mpango au mchakato wa kuanzisha viwanda vya kuzalisha *sponge iron* kutokana na vilima vilivyo nje ya Liganga. Tuna vilima vingine vingi sana nje ya Liganga ambavyo vina *deposits* za chuma kubwa tu kuweza kuanzisha viwanda vikubwa, kuweza kuzalisha *sponge iron* ambayo inahitajiwa kwa ajili ya uzalishaji wa mabati, nondo, misumari na kadhalika ikiwa ni mbadala ya chuma chakavu ambacho kimeadimika hapa nchini. Sasa kuanzisha viwanda hivi ni sawa lakini watu wengi sana watakaokuja kutumia fursa zinazotokana na uwekezaji huo. Tunategemea zaidi ya watu pengine 300,000 wataweza kuja na ku–*settle* Ludewa kwa ajili ya kushiriki kwa namna moja au nyingine kwenye viwanda hivi na uchimbaji wa migodi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini watu hawa watahitaji kula, watahitaji mpunga au mchele, nyama, maziwa yaani vitu ambavyo hatuvizalishi sisi Ludewa kwa wingi kuweza kulisha watu wote hawa. Kwa hiyo, utaratibu unaoambatana na kuanzisha viwanda hivi sasa hivi ni kwamba ni lazima kuanza kupanua kilimo cha mazao ya chakula pamoja na ufugaji ng’ombe wa maziwa na nyama. Lakini wananchi wale ni watu maskini sana hatutegemei kwa jembe la mkono na kwa utaratibu wa kawaida wataweza kuanzisha kilimo hicho na kama tunazungumzia *sponge iron* kwa kasi mpya yaani katika miaka hii miwili ijayo lazima viwanda hivyo vianze kufanya kazi, lakini watakula mawe?

Mimi naona mkombozi mmojawapo ndiyo benki kama hii ambayo hoja yake tunaizungumzia, kuwakopesha wakulima wadogowadogo wa Ludewa, kukopesha vikundi pengine hata *NGOs* na hata wakulima wa kati waweze kupata nyenzo za kuweza kulima na kuanzisha ranchi ndogo ndogo kwa ajili ya kuzalisha vyakula, nyama na maziwa kwa ajili ya watu ambao tunawategemea watakuja kwa wingi katika Wilaya ya Ludewa.

Sasa matarajio haya hayataweza kufanikiwa kama hatutakuwa na namna ya kuwawezesha wakulima wadogo wadogo waweze kupata mikopo. Na kule Ludewa sisi tunazalisha sana mahindi ambayo yatakuwa ni chakula kimojawapo kwa ajili ya watu kama hawa. Lakini nchi yetu ni ya milima sana hatuhitaji matrekta makubwa tunachohitaji ni nyenzo ndogondogo pamoja na matrekta madogo madogo ili watu waweze kulima kiasi cha ekari labda 10, 20 mpaka 30 bila kufikiria maeneo makubwa sana kwa sababu kwenye milima na mabonde huwezi kuwa na maeneo yanayohitaji matrekta makubwa. Kwa hiyo, sisi tunaiona benki kama hii na Serikali ikisaidia kuipa uwezo itakuwa imetusaidia sana wananchi wa Ludewa.

Lakini mfano wa pili unaoendana na huo, ni kwamba sisi tuna maeneo ya umwagiliaji makubwa sana, kuna eneo ambalo tayari upande wa Manda ambao Mto Luhuhu unaingiza maji katika Ziwa Nyasa tumekwishafanya upembuzi yakinifu, tume – *identify* ekari zaidi 1000 lakini tunataka wakulima wadogowadogo wazalishe mpunga, matunda na mbogamboga kwa ajili ya mgodi wa Mchuchuma kama utaaza mapema chakula kitatoka kule. Lakini wakulima wale watakuwa wadogowadogo wanaolima kwenye maeneo yao ili waweze kuzalisha chakula cha kutosha kwa ajili ya migodi lakini hawatakuwa na uwezo kama hakuna benki itakayoweza kuwakopesha.

Wamejaribu safari hii na fedha za Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete wakaambiwa upande wa kilimo hatutoi fedha. Mikopo hiyo si kwa ajili ya kilimo na wale maskini wako porini mbali sana na huduma hizi za kawaida na mijini kwenye benki, hawana uwezo wa kuja kukopa kwenye benki hizi nyingine ambazo nazo riba zake ni kubwa na masharti ni makubwa. Kwa hiyo, mimi naiona hii benki ingekuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa wananchi wale siyo wa Ludewa lakini Tanzania nzima.

Mheshimiwa William H. Shellukindo amezungimzia hata mazao ya biashara kama chai na kahawa. Sisi katika msimu huu kuanzia mwaka jana katika maeneo ya baridi tumeshaandaa vitalu zaidi ya saba kwa ajili ya chai na vitalu hivi jumla vitakuwa na miche zaidi ya 300,000 na wananchi hawa wadogo wadogo tunategemea walime ili kupanua kilimo cha chai ili kuongeza tija lakini na uzalishaji kwa zao ambalo tunauza nje ya nchi. Lakini wakulima hawa watakuwa ni wadogo, hawatakuwa na uwezo kungojea kipindi hiki cha miaka mitatu aliyoisema Mheshimiwa William H. Shellukindo yaani hela nyingi katika kilimo hicho itakuwa ni ndoto za Alinacha, wanahitaji benki ya aina hii iwasaidie wananchi kupanua kilimo cha chai.

Lakini kadhalika sisi tunalima kahawa. Safari hii vilevile tuna miche zaidi ya 300,000 ya kahawa ambayo tunategemea kwamba watagawiwa au kupewa wakulima wadogo wadogo wengi ili kuongeza uwezo wa uzalishaji wa kahawa ambao sote tunajua umuhimu wake katika pesa za kigeni. Lakini kama nilivyosema na wote tunavyoelewa, wakulima wadogo wadogo tunakubaliana kwamba hawana uwezo wa kuongeza kilimo cha kahawa au chai bila kupewa msaada wa namna moja au nyingine na kupewa mikopo na tunategemea kwamba benki hii itaweza kutusaidia sana.

Kama nilivyosema nilipoanza kuzungumza, mimi siyo mtaalamu wa uchumi lakini umuhimu wake nauona. Ndiyo maana napenda kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kuunga mkono zaidi ya asilimia mia moja. Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba benki hii inaimarishwa na inapewa mtaji wa kutosha ili wakulima wa Ludewa pamoja wa sehemu nyingine hapa nchini waweze kupata kipato zaidi ili kuongeza tija na kuleta maendeleo na fedha nyingi za kigeni katika nchi yetu.

Mimi naomba nirudie tena, naunga mkono kwa zaidi ya asilimia mia moja hoja hii iweze kuchukuliwa kwa uzito wake na Serikali yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Tunakushuru sana Prof. Raphael Benedict Mwalyosi. Kama nilivyosema mwanzo atafuatia Dr. Lucy Sawere Nkya na Mheshimiwa Paul Peter Kimiti ajiandae.

**MHE. DR. LUCY SAWERE NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii hoja iliyoletwa na Mheshimiwa William H. Shellukindo.

Niliposikia na kusoma huu mchanganuo wake na hii ripoti nilianza kujiuliza maswali mengi sana kichwani kwamba Tanzania kwenye miaka ya 1970 na 1980 mwanzoni tulikuwa tumejizatiti vizuri kuanzisha benki za kisekta ambazo zingesaidia Watanzania kujikomboa na umaskini. Mojawapo ikiwa ni Banki ya *CRDB*. Benki ya *CRDB* ilikuwa inalenga kuleta maendeleo vijijini, nikaanza kujiuliza hivi kulikoni? Kwa nini hii benki sasa imekuwa benki ya biashara na imeamua kubinafsishwa hailengi tena wananchi ambao wako vijijini ambao ndiyo wengi wanaochangia sana pato la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikarudi tena nikaanza kujiuliza *TIB* muda wote huo imekuwa tukiita ni Benki ya Raslimali Tanzania. Nikaanza kujiuliza, hivi ni raslimali ya nani wakati hii benki inawaangalia kwanza wawekezaji wakubwa wakubwa, wafanyabishara wakubwa wakubwa lakini watanzania tulio wengi hatuna hata taarifa kwamba hii benki ipo na inaweza ikamsaidiaje Mtanzania mzalendo ambaye ni maskini aliyepo kijijini. Kwa leo ndiyo mara yangu ya kwanza, naomba ni–*admit* tu kwa sababu *ignorance* siyo kitu cha kumdharau mtu, na–*admit* kwamba ndiyo nimeona kwamba kumbe benki hii inaweza ikatoa mikopo kwa wawekezaji wa kilimo.

Sasa nikajiuliza mwekezaji wa kilimo ni nani? Ni yule ambaye ana pesa nyingi ambaye anaweza akalima zaidi. Kwa hiyo, bado kabisa Benki ya Rasilimali ya Kitanzania haiwezi kumsaidia Mtanzania ambaye yupo kijijini aweze kujikwamua kutokana na umaskini hususan kipindi hiki ambacho nchi yetu na Serikali yetu imejipanga vizuri sana kutekeleza mpango au mkakati wa MKUKUTA. Lakini huu MKUKUTA utaishia kwenye mifuko ya watu ambao wana uwezo kujiondolea umaskini siyo wale ambao bado wako kijijini.

Mfano mdogo tu, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ameingina madarakani akatupa matumaini makubwa sana na wote tukafurahi na kwa nia njema ameahidi na ametekeleza ahadi yake kuleta pesa tunazoziita mabilioni ya Kikwete ili kila Mtanzania ambaye anataka kufanya shughuli yoyote aweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tu *experience* ya Morogoro. Benki ambazo zimepewa dhamana ya kufanya hiyo kazi wamekataa kuwakopesha wakulima wanaotoka zaidi ya kilomita 20 kutoka mjini Morogoro, sasa hizo hela zimekuja kwa ajili ya watu wa mijini tu? Kwenda kuwauliza wakasema Mama sikiliza kwa nia njema kabisa hawa watu wangesaidiwa lakini kwanza hawana mali ya kuweka dhamana na pili sisi hatuna pesa za kutuwezesha sisi kufuatilia hii mikopo huko vijijini zaidi ya kilomita 20 kutoka mjini, tukabaki tunajiuliza sasa inakuwaje?

Sasa Mheshimiwa William H. Shellukindo alipoleta hii hoja binafsi leo ikanikumbusha kwamba niliwahi kwenda China. Unapopita mtaani unaona Benki ya Ujenzi, unaona Benki ya Mawasiliano, Benki ya Masoko, Benki ya Mkulima, nikasema hivi kulikoni? Kwa nini na sisi tusianze kurudi nyuma tukaanza kuweka mikakati ya kuanzisha tena benki za kisekta kama kweli *we are very serious* katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie jambo moja kwamba wakulima wanajitahidi, wanalima lakini tatizo linakuwa ni masoko, na la pili tumekuwa tunawaambia wakulima kwamba ili tuweze tukapata dhamana kubwa ya yale mazao yao ni vizuri tukayaongezea thamani. Sasa hiyo dhamana ambayo tutawaongezea siyo mkulima anaweza, ni lazima aje mtu wa nje aongezee hapa hapa nchini na ataongezea kwa masharti yake anayoyaona mwenyewe na kwa matakwa yake.

Sasa nikasema kwamba kama Benki ya Mkulima ingekuwapo au kama Benki ya Raslimali kweli ingekuwa na mtandao wa kwenda mpaka kwenye ngazi ya Wilaya. Nafikiri kwa mtindo huu wa sasa ambao tunaanza kuhamasisha kuwepo na *SACCOS,* zingekwenda *beyond* kukopeshana ziamue sasa zitengeneze viwanda vidogo vidogo kwa msaada wa *SIDO* ili tuweze tukaongezea thamani yale mazao ambayo tunayalima kule vijijini. Hii haitawezekana kama hatutakuwa na benki ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nizungumzie ni kwamba nimekuwa nikiangalia hawa waliokopeshwa hapa nikajiuliza kweli mpaka na jina la Kifaransa na kadhalika je, hawa ni wawekezaji wa Kitanzania? Kama ni mtu ambaye amekuja kuwekeza Tanzania kwa nini aje akakope kwetu asikope kule kwake alete pesa hapa? Sasa mimi nachoomba ni kwamba benki zetu sasa zisije zikawa ni ngazi au tunasema kwamba ni kivuko cha mtu anakuja anatuambia anawawekeza halafu anatudanganya kwamba anaingia na pesa kumbe anatumia pesa ambayo ipo hapa hapa nchini kuja kuwekeza kwenye nchi yetu. Nafikiri ni suala la kuangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sasa nizungumzie kuhusu jinsi ambavyo wanawake tumekuwa ni waathirika wakubwa wa kushindwa kupata sasa uwezeshwaji wa pembejeo za kilimo. Tunakuwa na mfuko wa pembejeo na tumekuwa na benki nyingi, lakini mwanamke anayelima kijijini wengi wao wanalima kwa kutumia jembe la mkono. Sisi hatuna rasilimali ya kusema kwamba tunakwenda kuweka kama ni dhamana tuweze kupata mikopo. Zaidi ya hapo ni kwamba hata taarifa kwamba kuna uwezekano wa kuweka kukopa kama unaweza ukatimiza masharti moja, mbili au tatu hakuna. Nenda kwa mwananchi au mwanamke ambaye yupo Malinyi kule Biro hata gazeti halioni, Redio Tanzania haisikilizi, sasa hizi benki ambazo zinalundikana mijini, Dar es Salaam zinafanya nini kuhakikisha kwamba wale wanahamasishwa na wao waweze kupata haki yao ya kuja kukopa ili waweze kujikwamua kiuchumi? Ndilo swali ninalojiuliza. Nikafikia tena nikajiuliza hivi kweli ni watu ambao wangeweza wakatumika kupeleka hizi taarifa kwa wananchi?

Naomba nitoe sasa ushauri kwa hizi benki. Zile benki ambazo kwa nia njema kabisa wanataka kumsaidia Mtanzania wa kijijini hususan mkulima mdogo mdogo naomba wawatumie Maafisa Ugani wawafundishe na wawape semina waweze kuelewa kwamba kwenye benki zao kuna fursa gani ambazo zinaweza zikawasaidia wakulima wanaolima mazao ambayo yanaweza yakaondoa umaskini, watakopa namna gani na masharti ni yapi.

Sidhani kwamba kuna benki mpaka sasa hivi ambayo imefikiria kwamba wangeweza wakawatumia Maafisa Ugani na pale ambapo hakuna Maafisa Ugani naomba niseme kwamba tuna Maafisa wanaoshughulikia Elimu ya Watu Wazima wako vijijini hawafanyi kazi yao vizuri. Tuwatumie wale ili waweze kutumika pia pamoja na kumfundisha Mtanzania kusoma na kuandika, wamfundishe Mtanzania pia kumpa taarifa kwamba Mtanzania pamoja na kuondoa adui ujinga tuondoe na adui umaskini kwa sababu hata kujua kusoma ukashindwa kununua gazeti haitakusaidia.

Kwa hiyo, hawa na wao pia tuwatumie kwa mapana zaidi ili waweze kutoa elimu kwa wakulima kwamba kilimo bora kinakuwa hivi na vijarida vipo pamoja na kulima basi ulime zaidi tuweze kukopa na muweze kununua hata trekta kwenye kijiji, mnaweza mkaenda kuchukua mkopo hapa na tunaweza tukaenda na ninyi na tukawasaidia kuzungumza. Nafikiri watakuwa tayari kama hawatatumika. Sasa tufike mahali tukubaliane kwamba tunafanya kazi kama timu kupambana na umaskini na ambaye tunasema chachu kubwa ya kuondoa umaskini ni uwezeshwaji na huo uwezeshwaji basi kila Mtanzania afundishwe namna ambavyo anaweza akawezeshwa ili aweze kulima na kwa tija zaidi ili aweze kujikwamua yeye pamoja na kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiria hilo pamoja na kwamba kama tumefundisha kilimo kidogo shuleni basi na watoto wetu sasa waaanze kufundishwa kwamba Mtanzania huwezi kujikwamua kama hutakopa kwa sababu wengi tunaogopa kukopa kwa sababu hatukupata ile elimu ya kutuwezesha kujua kwamba kukopa ni lazima ili tuweze kupata maendeleo. Ukimzungumzia Mtanzania kukopa anakwambia unataka shamba langu liuzwe? Ni kwa sababu hakupata taarifa au elimu ambayo itamfanya aone kwamba kukopa ni sehemu mojawapo katika mchakato wa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba Serikali yetu sasa iangalie uwezekano wa kuanzisha benki ambazo zinashughulikia sekta za maendeleo, kilimo, masoko, ushirika, ujenzi, kwa sababu tunahitaji nyumba bora kwa sababu huwezi kupata pesa halafu huwezi kujenga nyumba ambayo ni ya bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo napenda pia kuipongeza Serikali yetu kwa kuanzisha mchakato wa MKUKUTA. Sasa huo MKUKUTA uboreshwe basi kwa kuangalia namna ambavyo walio wengi wanaweza wakapata *access* ya uwezeshaji wa mikopo ya masharti nafuu katika ngazi zote za nchi yetu.

Pili, napenda basi niseme kwamba nampongeza sana Mheshimiwa William H. Shellukindo kwa sababu ni wakati muafaka umefika sasa kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuanzisha benki ya wakulima pamoja na benki za aina nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya. Mheshimiwa Paul P. Kimiti atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Naibu Waziri Christopher Kajoro Chiza ajiandae.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kunipa nafasi angalau na nichangie kidogo kwenye hoja hii muhimu sana kwa maendeleo ya wakulima wetu. Kwanza kabla ya yote nataka kusema wazi kwamba naiunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii na mimi nishirikiane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Mbatia ambaye alikuwa ni kiongozi mwenzetu kwa muda mrefu na pia wengine waliopata majanga na ajali mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki pia nitumie nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa sana alioupata katika uchaguzi uliopita pamoja na viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi. Nawatakia kila la heri, sasa tumeanza upya kwa nguvu na ari mpya, tunategemea kwamba tutaleta mabadiliko makubwa sana katika Chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitumie nafasi hii kuwapongeza wenzetu wa *Tanzania Investment Bank*, wamefanya kazi nzuri sana kwa kipindi ambacho wamekuwa wakiongoza Benki hii, lakini bado kuna haja ya kufanya zaidi kuliko haya waliyoyafanya. Tutajaribu kuona namna ya kuweza kusaidiana ili kuweza kuimarisha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kilimo kama sayansi. Mimi ni mtaalam wa kilimo, kwa hiyo, ningependa mjue kwamba tunapozungumzia kilimo hatufanyi mzaha, tunazungumzia kama sayansi na sayansi huwezi kuiendesha bila kutumia utaalamu wa kisasa. Kama tutaendelea na kilimo chetu cha zamani haya tunayozungumza hatutafika huko tunapotarajia. Kuna mtaalamu mmoja anaitwa Rev. Thomas Mathus, miaka 200 iliyopita alisema dunia hii isipoangalia idadi ya watu itakuwa inaongezeka haraka kuliko chakula kinavyopatikana na mwisho wake ni maafa kwa dunia. Lakini wataalamu wakaja wakasema hapana, ulimwengu utabadilika, tutatumia kilimo cha sayansi ili tuweze kuzalisha chakula kingi katika eneo dogo. Wakasema tutakuthibitishia hivyo usiwe na wasiwasi lakini hali ninayoiona bado haijabadilika sana, bado ushauri wa Rev. Thomas Mathus, ni vizuri tukaukumbuka kwa sababu hali ambayo naiona haiendani na matarajio tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema kilimo ni sayansi. Kwa sababu bila kutumia utaalamu hutarajii kupata mavuno kama ambayo ungeweza kuyapata kama ungetumia sayansi kidogo. Kilimo ni nini? Kilimo ni mbolea, maji, zana za kisasa na kilimo ni kuhakikisha kwamba unatumia kila aina ya dawa inayowezekana ili angalau kuweza kupigana na wadudu ambao wanaangamiza mazao yetu. Vyote hivi vina gharama, ukiweza kuendesha kilimo bila kuangalia gharama hutafika mahali popote. Sasa tuangalie wakulima wetu hali yao ya mazingira. Bei ya mbolea inapanda kila siku na mkulima huyu ambaye tunategemea anunue mbolea hiyo kwa bei ambayo tunasema ina ruzuku, haiwezekani. Mwaka juzi nilijaribu mimi mwenyewe kwenda mpaka *TIB* kuona uwezekano wa kupata kibali cha kuagiza mbolea kutoka Ujerumani. Mfumo wa uagizaji wa mbolea katika nchi yetu lazima utazamwe upya kwa sababu mtindo uliopo pamoja na ruzuku ambayo tutakuwa tunaitoa mwaka hadi mwaka, bei ya mbolea inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza ndani ya Bunge kwamba kulikuwa na uwezekano wa kuingiza mbolea hapa tena *UREA DAP*, *CAN* kwa shilingi 13,000/= mpaka Sumbawanga mpaka Bukoba kwa mfuko wa kilo hamsini. Kilichokuwa kinatakiwa ni kwa Serikali kutoa *guarantee*, tuagize mbolea nyingi kwa wakati mmoja kuliko mtindo wa sasa kila mtu anajiagizia tani elfu moja, elfu mbili. Hapa hatuwezi kupata mbolea kwa bei ya chini kama tutakuwa tunaagiza kidogo kidogo. Sasa nashukuru, nasikia Wizara ya Kilimo inaanza kuliangalia hilo, lakini nataka kusema kwamba bila kutumia mbolea, sayansi ya kisasa, kilimo chetu kitakufa.

Kwa nini nasema hivyo? Mkulima wa kawaida ili aendane na matarajio ya kilimo cha kisasa lazima tuhakikishe wanapata zana kwa sababu majembe ya kukokotwa na ng’ombe siku hizi bei yake imepanda sana. Zamani tulikuwa tunayapata kwa Sh. 70,000/= au 80,000/=, lakini sasa yanafika mpaka Sh. 200,000/=, mkulima wa kawaida atapata wapi? Lazima awe na utaratibu wa kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali na chanzo kimojawapo ni kuwa na benki yake ambapo atakuwa na uhakika. Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi kimesema kwamba, mkulima huyu ambaye hana kitu lakini ardhi anayo, tungekuwa na utaratibu wa kurasimisha mali zake zikatumika katika kupata mikopo, tungefika mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, ianze utaratibu wa kurasimisha mali za wakulima wetu. Nyumba anakuwa nayo na ana ardhi yake, hizo ndizo mali zake, akipata thamani ya vitu hivyo ni rahisi kuweza kukopesheka. Sasa katika kilimo chetu ambacho tunategemea kiwe cha kisasa, tunategemea sasa badala ya kuendelea kutumia jembe la mkono tuingie katika hatua ya pili ya plau na matrekta na haya ndiyo njia peke yake itakayofanya vijana warudi vijijini. Hiki kilimo cha kutumia jembe tangu asubuhi mpaka jioni vijana wanaogopa na ndiyo wanakwenda mijini. Matokeo yake watabaki wazee peke yao na wazee wakibaki peke yao ndiyo hali ya kuwa na chakula kidogo ndani ya nchi kwa sababu wakulima watakuwa hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nataka nitoe kama angalizo kwa sababu tunapokwenda huko tusipoangalia tutakuja tujikute wazee wote ndiyo wamebaki vijijini, vijana wamehamia mijini, lakini tukiongeza teknolojia kidogo ndani ya kilimo sifichi, vijana wote watabaki vijijini. Nachukulia mfano, katika Mkoa wetu wa Rukwa, kwa

kweli nawashukuru wakulima wa Mkoa wa Rukwa, wanatumia zaidi plau za kukokotwa na ng'ombe, wanazitumia sana kwa sababu hata vijana wakitoka shuleni wanaona ile siyo bughudha bali ni kazi ya kawaida. Lakini angekuwa anarudi shuleni, halafu anaanza kulima tangu saa sita mpaka jioni angeona hii ni bughudha, kwa nini nasumbuka, lakini vijana wenyewe wanalima tena kwa furaha kwa sababu wanatumia nguvu kazi ambayo tunatumia ya wanyama. Sasa teknolojia inapoongezeka kidogo hali ya uzalishaji inakuwa nzuri lakini haiwezi kuongezeka bila kuwa na mtaji wa kumwezesha anunue zana hizo, anunue mbolea, ahakikishe kwamba maji yapo na wakati mwingine kujenga malambo ili tuweze kumwagilia. Katika hali hiyo, nadhani ni vizuri tukaliangalia katika hali ya kutaka kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo matatu ambayo nadhani ni vizuri tukayaangalia. La kwanza, ni kuanzisha Benki ya Kilimo. Hii ndiyo itakayojibu matarajio haya. *TIB* mwenye hisa mkuu ni Serikali karibu asilimia tisini na tisa. Kwa nini Serikali hii hii isianzishe benki za wakulima? Tuwe na matawi kila Mkoa na kama inawezekana kwa kila Wilaya, ili tuwe na uhakika kwamba tunaweza kuwakopesha wakulima wetu na tuwe na utaratibu wa kurasimisha mali zao, MKURABITA ianze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nishauri sasa kuwepo kwa utaratibu mzima wa kukopesha wakulima mbolea na zana za kilimo kupitia kwenye benki hizo. Itakuwa ni rahisi kuliko kuwa na mfumo tofauti kabisa. La tatu, *TIB*, iongezewe mtaji ili angalau wakati tunajenga utaratibu wa kuanzisha benki kama hii tuwe na uhakika *TIB* tunaiwezesha ili iendelee maandalizi yote ya kuanza kuwakopesha wakulima wadogo wadogo. Hiyo itakuwa ni njia peke yake itakayosaidia ili wazo hili alilolileta Mheshimiwa Shellukindo liweze kutekelezwa kwa nguvu na naomba kabisa hili lipewe msukumo wa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka kumpongeza Mheshimiwa Shellukindo, ameanza vizuri na sisi tutaunga mkono hoja yake na nina imani Serikali itachukua kila aina ya utaratibu ili kuanzisha benki ya wakulima vijijini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, nitajitahidi sana nizungumze kwa kifupi kama ulivyonitaka nifanye hivyo. Lakini naomba nitumie nafasi hii nami kwa sababu ndiyo nasimama kwa kuwa na muda wa kutosha ambao naweza kutoa salamu, basi naomba nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Salome Joseph Mbatia aliyekuwa Mbunge mwenzetu na Naibu Waziri na naomba tu familia yake istahimili hilo kwamba haya ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Pia niwape pole Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao walipata ajali katika kipindi hiki. Namwomba Mwenyezi Mungu pia awape afya njema na wale ambao wapo Bungeni basi waweze kurejea Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa wale wote ambao walipata ajali juzi kule Mbozi katika kijiji cha Nanyala na

katika Jimbo langu la Uchaguzi. Wale waliofariki basi niziombe familia zao zistahmili na wale ambao wamepata majeraha basi Mwenyezi Mungu awaponye mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nitoe pongezi kwa Chama cha Mapinduzi kwa kufanya uchaguzi vizuri na kumaliza vizuri. Pia niwapongeze wale wote waliochaguliwa katika nyadhifa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo naomba nichukue nafasi hizi niweze kuchangia kwa ufupi sana juu ya hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Shellukindo. Nami niungane sana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Shellukindo kwa kuleta hoja yake hapa Bungeni. Lakini pia naomba niseme sana nikiitumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo iliyotuweka sisi wengi wa Chama cha Mapinduzi madarakani na baadaye juu ya hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Shellukindo. Nami niungane sana na wenzangu kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Shellukindo kwa kuleta hoja yake Bungeni. Naomba niseme sana nikiitumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndiyo iliyotuweka sisi wengi wa Chama cha Mapinduzi madarakani na baadaye kukiwezesha Chama chetu kuunda Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Shellukindo ni ya msingi sana kwa sababu wenzangu wamesema. Kwa hiyo, naweza nisiwe na mambo mengi sana kwa sababu mambo muhimu wenzangu wameyasema ila nitakachofanya pengine ni kusherehesha au kutia msisitizo ili tuone umuhimu wa kuikubali hii hoja ya Mheshimiwa Shellukindo ya kuanzisha Benki ya Wakulima. Ni kweli mwaka 1997 benki ya *CRDB* iligeuzwa na kwa maana hiyo iliacha sana kutoa misaada au mikopo kwa wakulima moja kwa moja pamoja na kwamba wanaendelea kutoa lakini ni ya kibiashara zaidi kuliko kuwasaidia wakulima na badala yake ikaanzishwa benki hii ya *TIB* ambayo kimsingi ilikuwa na yenyewe isaidie wakulima lakini naomba pia niungane na Mheshimiwa Shellukindo kwamba benki hii kwa sehemu kubwa haiwasaidii wakulima. Nadhani Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi kwamba ni wakulima kwanza wachache sana kama wapo ambao wanaijua benki hii ya *TIB*. Naamini kwa sekta nyingine inafanya vizuri lakini kwa wakulima ni wachache sana ambao wanaweza kuijua kwamba ipo na masharti yake ni ya kibiashara, siyo ya kuwasaidia wakulima wenyewe. Lakini pia nilikuwa napitia kitabu hiki ambacho Mheshimiwa Shellukindo ametuonyesha, ukisoma ukurasa wa (5), wanasema, naomba ninukuu: "Katika mwaka 2006, *TIB* iliendelea na matayarisho muhimu ya kuyabadili kuwa Benki ya Maendeleo ya Taifa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nimeshindwa kuelewa, huku ilikuwa Benki ya Uwekezaji, sasa tunataka ibadilishwe iwe Benki ya Maendeleo ya Taifa, lakini bado mkulima hatajwi popote hapa kwamba anaweza sasa kunufaika zaidi na kuanzishwa kwa benki hiyo ambayo inakusudiwa na hayo. Kwa hiyo, bado mimi naendelea kusisitiza kwamba naiunga sana hoja ya Mheshimiwa Shellukindo kwamba tuangalie uwezekano wa kuanzisha benki itakayowalenga wakulima wetu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, sura ya tatu, naomba tena kwa idhini yako ninukuu, anasema: "Kilimo ndiyo msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika *modernization* ya uchumi wa Tanzania". Kilimo cha

kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa. lakini wakulima wetu kwa wastani wanalima vishamba vidogo vidogo, wanategemea zana duni za jadi na hasa jembe la mkono. Tunasema vilevile kwamba utazamwe uwezekano wa kutoa ruzuku ya mbegu bora ili kuwavutia wakulima pamoja na pembejeo za kilimo. Lakini ni ukweli kwamba wakulima wetu wataendelea kulima vishamba vidogo vidogo, wataendelea kutumia zana duni kama majembe ya mkono lakini pia wataendelea kutokulima mashamba makubwa kwa sababu wanakosa mbolea na hawakosi hivi vyote kwa sababu ya kupenda isipokuwa tatizo hatujawapa uwezo. Chombo ambacho kinaweza kuwasaidia ili waweze kupata mikopo itakayowawezesha kulima vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kule Mbeya na kwenye Jimbo langu kwa ujumla kuna tatizo kubwa sana la mbolea. Mahitaji ya mbolea katika Wilaya ya Mbozi kwa mfano ni tani takriban elfu thelathini lakini mbolea ambayo tunapata ni tani elfu sita. Sasa tani elfu sita naamini kama wakulima wetu wangekuwa na chombo muhimu cha kuweza kukopa kwa riba nafuu wangeweza kujitegemea wao wenyewe na kwa maana hiyo wangeweza kupata uwezo wakakopa kwenye mabenki na wangeweza kununua mbolea ambayo ingewatosheleza kuweza kulima kwa tija zaidi kuliko ilivyo sasa. Ni kweli kwamba Serikali inatoa ruzuku lakini ruzuku inayotolewa tunapata kama nilivyosema asilimia chini ya ishirini ya mahitaji ya mbolea yote. Sasa hapa ni kweli Serikali ione umuhimu wa wazi kabisa ili tukubaliane na wazo la Mheshimiwa Shellukindo la kuweza kuwapa wananchi chombo ambacho wanaweza kutumia zaidi kwa ajili ya kukopa. Lakini pia hata hizi pesa ambazo ni maarufu kama pesa za Mheshimiwa Rais, wanasema pesa za JK, ni wakulima wachache sana ambao wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kule kwangu Mbozi watu wanaolima ni zaidi ya laki moja lakini watu waliofaidika na mikopo hii pamoja na kwamba ni mpango mzuri ni wachache. Mikopo hii haitoshelezi, watu wanaoweza kukopa ni takriban elfu mbili. Sasa kama watu wanaoweza kukopa ni elfu mbili kati ya watu laki moja wanaolima, bado hatujamsaidia mkulima inavyostahili. Kwa hiyo, bado kuna umuhimu wa chombo kingine kuwepo. Juzi nilikuwa Cairo na tumezunguka sana mjini Cairo kama wenzangu wengine waliotembea katika nchi nyingine mbalimbali. Pale kila mahali unapokwenda unaona benki zinazohusika na mikopo kwa ajili ya wakulima. Benki mahususi kwa ajili ya wakulima pamoja na kwamba kuna benki zingine za sekta mbalimbali, lakini benki zinazomjali mkulima, zinazotoa mikopo nafuu kwa wakulima zipo sehemu nyingi sana pale Mjini Cairo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba Serikali ikubaliane na wazo hili na mimi ningewashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu wale wote waliochangia na ambao hawakuchangia, na Serikali tuone umuhimu wa kuchukua hili wazo ili tuweze kuanzisha benki ambayo itawasaidia wakulima wetu ili waweze kulima kwa tija. Kama kweli tuna nia ya kuleta mapinduzi ya dhati ya kilimo, lazima tuwape wananchi wetu chombo ambacho kitaweza kuwasaidia ili waweze kuwekeza vizuri na kulima kwa tija zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, naomba niseme kwamba naiunga mkono hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Shellukindo ili Serikali ifikirie kuanzisha benki kwa ajili ya maendeleo ya wakulima vijijini. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHESHIMIWA MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache. Kwanza, nimpongeze sana ndugu yangu Shellukindo kwa kuleta hoja hii ili tuizungumzie, lakini bila kusahau ningependa na mimi kutoa rambirambi kwa mwenzetu Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Mbatia na Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia tu machache kuhusu benki hii. Ukiangalia kwa watu wengi benki hii ni ngeni. Pamoja na kwamba ni benki iliyopo hapa Tanzania kwa muda mrefu, lakini ningependa kuzungumzia huduma zinazotolewa na benki hii. Wengi wamezungumzia masuala ya kilimo na katika benki zetu zinazotoa mikopo, nasema kwamba wanaofaidika ni wale watu wakubwa wenye uwezo, bado Serikali haijatafuta namna ya kuwawezesha watu wa vijijini kupata mikopo. Ndiyo maana umaskini unazidi na ndiyo maana tofauti inatokea, tofauti ya walionacho na wale wasionacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu umaskini unazidi kuwa mkubwa kila siku na wenzangu wamezungumzia sana kilimo na mimi ningependa kuzungumzia suala la wafugaji kusaidiwa mikopo. Naona Serikali haiwatambui kabisa wafugaji na naona hakuna mkopo unaotoka mahali popote unaokwenda kwa wafugaji na wafugaji wao wanafuga katika maeneo ambao hayalimiki. Kwa hiyo, ukizungumzia kila siku kilimo, tujue kwamba kuna wananchi ambao wapo katika maeneo ambayo hayalimiki lakini ni mazuri kwa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kusema kwamba katika benki hii tutafute namna ya kuwasaidia wafugaji nao, wanaweza kufungua ranchi na kuna ranchi nyingi ambazo hazitumiki lakini bado Serikali inazihodhi kwa nini wasipewe hawa wafugaji mikopo ili waendeleze hizo ranchi? Kama tunataka umaskini upungue, matajiri waliopo nchini hawawezi kupunguza umaskini kama wao ndiyo wanazidi kupewa mikopo kila siku. Umaskini utapungua endapo watu wa hali ya chini watasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vigezo vingi ambavyo vinawanyima watu wa hali ya chini wasipate mikopo, hivyo vigezo ndiyo viangaliwe ili watu wa chini waweze kupata mikopo.

*(Hapa kengele ililia)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Lekule Laizer kwa mchango wako, Mheshimiwa Kimbita pia alinithibitishia kabisa kwamba kwa dakika kama za Mheshimiwa Lekule Laiser ujumbe wake utakuwa umefika.

**MHE. FUYA G. KIMBITA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Wenzangu wengi wamekwishayazungumzia ni masuala muhimu na ya msingi kabisa, mimi katika kutoa pole na pongezi nimekwishafanya hivyo wakati nilipoongea wiki iliyopita. Sasa naomba niende moja kwa moja kwenye suala lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mzee Shellukindo - Seneta kama ulivyomtaja, kwa hoja yake nzuri. Niseme ni suala la kusikitisha, ukiangalia hata hizi kumbukumbu alizotupa Mzee Shellukindo hapa kuhusu mikopo iliyotolewa ya kilimo. Katika miaka minne mikopo iliyotolewa au miradi 186 ya kilimo ni 17 tu. Lakini ni kilimo cha watu gani hawa? Ni wale wakubwa, hawa wadogo je? (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tuondoe ile dhana inayosema maji hufuata mkondo, kwa maana ya kwamba wale walionacho ndiyo watakaoongezewa, je, watu wadogo tutawapeleka wapi? Wakulima wadogo tunawapeleka wapi katika Taifa letu na katika nchi yetu hii kama hatutawafikiria na kuwajadili. Wenzangu wengi wamekwishazungumzia, ukitembea katika nchi nyingi sana yapo mabenki ya kisekta. Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya amekwishataja, Mheshimiwa Zambi ametaja. Hawa wenzetu waliopata hisa katika benki ya *NMB, RABO Bank*, kule kwao nimetembea, wao ni watu wa kilimo kabisa. Sasa wanapokuja hapa nadhani kwamba kuna kigugumizi, nadhani kwa kuwa kuna jinsi nyingine ya kupata fedha na faida za haraka bila ya kupitia kwenye kilimo. Kwa hiyo, huenda nao pia wasijikite tena huko kwa sababu wengi wanaogopa. Sasa ningeomba tuache kigugumizi, tukae tuzungumze, tujadiliane na Serikali, tuweze kuanzisha benki ya wakulima wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Laiser amezungumzia na wale ndugu zangu wafugaji. Tunapozungumzia kilimo tunamaanisha ni wakulima wa kilimo cha mazao na kilimo cha ufugaji. Hicho ndicho kilimo, ufugaji na kilimo cha mazao. Kwa hiyo, na wafugaji nao tuwazungumzie, tuwajadili na tuangalie ni jinsi gani tunaweza kuwasaidia ili tuweze kuwaendeleza kutoka pale walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuunge mkono sana Mheshimiwa Shellukindo kwa hoja yake nzuri. Ni hoja mahususi kabisa, tumefikia mahali tuyazungumze haya masuala kwa uwazi na bayana kabisa, tuweze kuwasaidia wakulima wetu wadogo wadogo kwa sababu hapa ni wale wakulima wakubwa tu ndiyo wanapata hizi pesa. Ukiangalia orodha ni kampuni hizo hizo zinajirudia mwaka hadi mwaka, sasa hiyo tuachane nayo, aidha, kama itakuwa ni *TIB* au tutaanzisha Benki maalumu ya maendeleo ya kilimo. Wenzetu Kenya hapo wana benki ya kilimo, licha ya kuwa eneo lao kubwa la nchi ni jangwa, sisi tuna eneo kubwa zaidi linalofaa kwa kilimo kwa nini tusiwe na benki kama hiyo ili utaalamu wa Ugani tunaouzungumzia tuupeleke kwa wakulima wetu uweze kuzaa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kwamba tuwafundishe wakulima kilimo cha kisasa. Kwa mfano, kuna kule kutumia vitu kama chezo badala ya plau ili maji yaweze kukaa ardhini, vizuri. Kuna *crop population,* lakini yote haya hayatakuwa

na tija kama hatutawasaidia hawa wakulima kwa maana ya kuwapatia mikopo ili waweze kulima kilimo ambacho kitakuwa na tija zaidi, na mazao mengi ukiangalia muda wake wa kuvuna ni mrefu kidogo. Kwa mfano, wale wakulima wangu wa kahawa, hii kahawa mpya bora tunayoizungumzia, miche mipya bora ya kilimo, inahitaji miaka miwili na nusu hadi mitatu, lazima tuweze kuwasaidia hawa wakulima waweze kupata mikopo ya muda mrefu ambayo itawasaidia. Na kule kwetu unajua tuna uhaba wa ardhi ndiyo maana tunaomba omba ardhi kwenu, lakini vile vishamba vidogo tunavilima ambavyo ni kama *plots*, lakini tukiwasaidia fedha kiasi wataweza kulima na kuboresha kilimo chao vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na pia naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, napenda nimshukuru mtoa hoja Seneta Mheshimiwa Shellukindo, kwa sababu hoja kama hii nakumbuka sisi tumewahi kuwa nayo katika Wizara ya Kilimo, lakini niseme kwamba hatukuwa tumeifikisha ngazi aliyoifikisha Mheshimiwa Shellukindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwamba nilipokuwa nasoma hoja hii nilipata kuchanganyikiwa kidogo kwa sababu hoja ukiisoma inazungumzia *TIB*, lakini ukija kule mwisho unaona kabisa kwamba hoja ambayo Mheshimiwa Shellukindo anaiweka mbele yetu ni hoja ya suala zima la *Agricultural Financing* (suala la uwezeshaji) ambayo nadhani kwa kweli haina mjadala. Hoja hii naonekana wazi na labda nianze kusema naiunga mkono hoja, pamoja na kwamba huko mbele nitasema kwamba inahitaji mchakato wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naunga hoja hii, naomba nitoe maneno machache tu ambayo pamoja na hayo kwa njia nyingine nitakuwa pia namsaidia Naibu Waziri ambaye atatoa ufafanuzi. Huko nyuma kwenye miaka ya sitini wale wanaokumbuka nafikiri 1965-1967, tulikuwa na benki inaitwa *TRDB* ambayo sasa hivi ndiyo tunaita *CRDB*. Ni jina limekuwa *transformed*, lakini ukisoma vizuri mabenki yote haya huko nyuma yalikuwa yanalenga uwezeshaji wa wakulima. *TRDB* ilikuwa inaitwa *Tanzania Rural Development Bank*, lakini U-*rural* uliomo katika misahafu ile ya *TRDB by large* ulikuwa unalenga wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninacho kitabu kinachozungumzia mabenki na uwezeshaji wa wakulima na hasa hasa ikilenga *TRDB*. Kama Mheshimiwa Shellukindo angekuwa ametupa nafasi ya kutosha na tukaelewa hoja hii nina hakika kabisa Wabunge wengi wangechangia. Sasa naomba nianze kwa kusema nitakipiga fotokopi hicho kijitabu kama kutakuwa na muda. Nina hakika kutakuwa na muda kwa sababu hoja yenyewe ni nzito na ni nzuri. Nitakipiga fotokopi hicho kijitabu nimpatie Mheshimiwa Shellukindo ikiwezekana Wabunge wote waone *TRDB* ilivyokwenda ikawa *transformed* kuwa *CRDB* na kwamba malengo yalikuwa ni yapi na wakati wa kujadili tuweze

kuangalia hivi ni kwa kiasi gani tumelizungumzia hili suala la uwezeshaji wa wakulima. Kwa hiyo, naahidi kwamba nitatoa hicho kijitabu ili kitusaidie katika mijadala ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba nizungumzie hili. Masharti yanayotolewa na mabenki kwa wakulima kwa kifupi ni kwamba hayawezekani kwa mkulima mdogo, maana yake hili hatuna haja ya kulijadili. Wakulima wengi wamekuwa wanashindwa, tunasema hawakopesheki kwa sababu ya yale masharti ambayo yapo katika mabenki haya ambayo ndiyo yanatakiwa kuwawezesha wakulima. Maana yake sasa ni nini hapa? Ninavyoona Waheshimiwa Wabunge wengi wanachotwambia ni kwamba umefika wakati sisi Serikali mahali pengine kufanya maamuzi ya makusudi. Tumekuwa na watu wengi ambao wamekuja kwenye masuala ya kilimo katika zana kama matrekta. Makampuni mengi yamekuja na yanasema sisi tupo tayari, kama ninyi mnaingiza matrekta mia mbili mpaka mia tatu kwa mwaka kutokana na uwezeshaji mdogo, basi sisi tupo tayari kuleta matrekta hata elfu mbili kwa mara moja ili kuwawezesha. Lakini ukiliangilia hilo tena utakuta tatizo kubwa kama atakavyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. Ni kwamba kuna suala la *guarantee* ndani yake ambalo linahitaji mchakato mzito. Sitaki kuingilia suala hili la *guarantee* kwa sababu nina hakika Mheshimiwa atalielezea, lakini nataka kuonyesha tu kwamba watu wengi wamekwishaona umuhimu wa Serikali kufanya mamuzi ya makusudi ili kuweza kuwanusuru wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia Mfuko wa Pembejeo. Mfuko huu si Benki, lakini ninavutwa kuuzungumzia. Mheshimiwa Mbunge alisema hivi Mfuko wa Pembejeo unawasaidia watu gani? Wakati najibu swali Bungeni humu nilijaribu kuwataja na sitarudi kuwataja walengwa Mfuko huu. Lakini ninalotaka kulizungumzia kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, wakati nakwenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge muuliza swali alisema naomba kuongezea kipengele cha udhamini wa walengwa kwa kutumia Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niseme Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri za Wilaya tumezikubali kama tunavyowakubali watu wengi kudhamini waombaji. Waombaji wengi wanapokuja wanaambiwa lazima uwe na mali isiyohamishika, lazima uwe na hiki. Lakini suala hilo ni la kukariri vile vigezo au wale wadhamini. Mimi nimesema na naomba tulielewe kwamba utaratibu huu unaweza ukabadilika siyo lazima uwe na nyumba tu ndiyo uende ukakopeshwe. Halmashauri za Wilaya zikikubali kuwakopesha watu wanaotaka kuanzisha Vituo vya kuanzisha matrekta tunaweza tukakubali. Tatizo lililojitokeza ni kwamba Halmashauri za Wilaya zenyewe zinasita, zinasema tukikopesha wakishindwa kulipwa, Madiwani watakuja juu, Serikali itauza mali zetu. Hivi Serikali inauza mali zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba niwaachie changamoto hiyo kwamba wasiogope, hebu jaribuni! Siamini kama utakuta Serikali ije iseme tunauza mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, Halmashauri za Wilaya zinayo nafasi hii pia kuweza kutusaidia kuwadhamini wakulima na kuwafungua macho badala ya kuwaachia wao tu wanahangaika kila mahali wakienda wanakuta mambo haya hayawezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo nigusie suala la MKURABITA, sijui dakika zangu ni ngapi? Maana naona Mwenyekiti ananitazama. Lakini suala la MKURABITA nadhani linahitaji kufanyiwa kazi ya ziada. Nataka nitoe mfano tu kwamba hii siyo nadharia inawezekana. Sisi tumejaribu kwa kutumia sheria ile ya ardhi nadhani namba 5. Kule Mufindi ndiyo tuliweka kama *model,* na wakulima wachache wakapimiwa mashamba yao na wakapata hatimiliki za mila na baadhi yao wamepata mikopo ya matrekta. Maana tatizo lingine kubwa lililopo ni kudhaminiwa. Mabenki yanasema hao watu hawakopesheki, nadhani ndilo suala zima tunalolizungumza kwamba watu waweze kukopesheka yaani wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili la MKURABITA nadhani ni hoja nzuri aliizungumzia vizuri sana Mheshimiwa Paul Kimiti na mimi nataka tu kuliunga mkono kwa sababu tayari kuna mifano ya kujifunza. Kama mtu ameweza kupima shamba lake akajipatia hatimiliki na akapata mkopo wa trekta basi hii *model for replication* nadhani ni vizuri tuendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sijasikia kengele, kwa hiyo, mimi nitaendelea tu. Lipo suala ambalo Mheshimiwa George Simbachawene amelizungumza. Naomba nilirudie tena. Ni suala la Mfuko wa Pembejeo, kwa kweli ninavyoliona mimi na kama nilivyosema katika majibu yangu leo mkisoma majibu yale ya sehemu (c) nimesema kwamba inaonekana Mfuko huu haujajinadi kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo matatizo mengi. Tatizo la Mfuko huu wa Pembejeo lingine ni mtaji mdogo na tatizo lingine ni hilo hilo nililolisema kwamba pamoja na mtaji mdogo, pamoja na wakulima kutouelewa vizuri Mfuko hata wale ambao wameuelewa bado niseme kwamba dhamana ni tatizo. Kwa sababu Mfuko huo pamoja na kwamba masharti yetu tumeweka ni madogo sana, asilimia 8 ndiyo riba na unalipwa kwa miaka mitano. Lakini matatizo yanakuja kwamba huyo mkulima aliyepo kule kijijini hata hiyo dhamana tunayoizungumzia hana. Lakini tumeruhusu kupitia *SACCOS*, waweze kutumia Muungano wao *SCULT* wakope na mifano hai ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuanza kutaja, lakini ipo mifano hai ya wakulima ambao wametumia utaratibu huo na wakakopeshwa. Sasa ningeomba pamoja na Mfuko wa Pembejeo kujinadi kwa wakulima kueleza masharti yaliyomo, basi na Waheshimiwa Wabunge na wao watusaidie kwa sababu wao wanajua ni watu gani tunaweza tukawatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa William Shellukindo, lakini Serikali iwe na nafasi kubwa katika mchakato utakaofanywa na katika benki hiyo tunayotarajia kuunda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa William Shellukindo, katika hoja hii muhimu iliyoletwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipoambiwa kwamba kuna hoja inayohusu *TIB* kwa kweli maandalizi yetu yalikuwa tofauti, kwa sababu Wizara ya Fedha kwa kweli haijihusishi moja kwa moja na kilimo, ukiacha kazi ya kutafuta fedha, Wizara haijihusishi sana na mambo ya kilimo, sisi kazi yetu ni kukusanya fedha na kuzigawa Serikalini kwa kadri ambavyo Serikali inaamua. Tungejulishwa kwamba hoja nzima ni kwa ajili ya kuja kuzungumzia uanzishwaji wa Benki ya Kilimo tungekuwa tumejiandaa vizuri. Nadhani hata mchango wetu ungekuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nitajaribu kuchangia kwa kadri nitakavyoweza. Benki ya *TIB* iliundwa mahususi kwa ajili ya kutoa mikopo ya uwekezaji yaani *investment* iwe *industrial,* iwe kilimo lakini kilimo kwa maana kwamba ni kilimo kikubwa *large scale* na maeneo mengine. Katika mchakato wetu wa Serikali tuna aina kadhaa za Benki. Tuna *CRDB* ambayo kwa kiasi kikubwa kwa kweli kama mwenzangu Mheshimiwa Christopher Chiza alivyozungumza tangu mwanzo ilipoundwa mtazamo mkubwa ulikuwa kwamba ndiyo Benki ambayo ingesaidia sana kilimo, na mwanzo ilikuwa Tanzania *Rural Development Bank*, lakini baadaye ikabadilishwa ikawa *Credit and Rural Development Bank*, lakini nadhani baadaye wakaja wakabadilisha tena na sasa inaitwa *CRDB Bank Ltd.* Kwa hiyo, ina maana kwamba yale majukumu ya mwanzo ambayo iliyokuwa imepewa *CRDB* ya kuwa benki ya kushughulikia kilimo kwa kuiita *CRDB Bank Ltd*. majukumu hayo sasa hayaonekani moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, benki ambayo kwa kweli Kiserikali ingejishughulisha sana na kilimo ni *CRDB.* Lakini kwa sasa hivi *CRDB* ni *hundred percent private.* Kwa hiyo, Serikali haiwezi kutoa *instructions* kwa *CRDB* kwamba wafanye nini? Tunazo *shares* pale asilimia 30 ambazo zipo *owned* na Serikali ya Denmark, lakini kuna mchakato unafanyika kuona kama Serikali inaweza ikachukua *share* zile ili ziuzwe kwa wananchi na nyingine zibakie katika mikono ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachozungumzwa au kinachoombwa kama nimeelewa ile *paper* ya Mheshimiwa William Shellukindo vizuri kwa kweli tunazungumzia *Microfinance.* Ukishazungumza wakulima wadogo maana yake ni *Microfinance,* na *Microfinance* katika *charter* ambayo tuliundia *TIB* si kazi ya *TIB.* Kwa Benki zilizopo sasa hivi hapa nchini, *microfinance* ni kazi ya *NMB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *NMB* kama mnavyofahamu inafanyiwa *restructuring* ili kuona jinsi gani inaweza ikajihusisha kwenye mambo ya mikopo hiyo. Nadhani tunachoweza kufanya ni kuchukua mawazo yote ambayo Mheshimiwa William Shellukindo ameyatoa ili tuweze kuona ni jinsi gani kati ya *CRDB* na *NMB* hii kazi ya *Microfinance* ambayo pia itahusu wakulima wadogo inaweza ikafanyika. Ili tuiachie *TIB* inayokusudiwa kuwa kama *ADB* ya Tanzania au *Africa Development Bank* ya Tanzania ndiyo *TIB* ambayo tunajaribu ku-*transform* itakavyokuwa. Kwa maana

nyingine ni Benki ambayo tutaiwezesha kupata mtaji wa kutosha ili iweze kutoa mikopo ya muda mrefu kwa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Paul Kimiti amezungumza kwamba ukitaka kupata mkopo wa miaka mitano au wa miaka 10, benki nyingi tulizonazo haziwezi. *TIB* ndiyo benki ambayo tunakusudia kui-*transform* ili iwe benki ambayo inaweza ikatoa mikopo ya muda mrefu. Kwa hiyo, tukisema tuzichanganye kazi za mikopo ya muda mrefu na kazi za mikopo ya *Microfinance* tutakuwa tunachanganya sukari na chumvi, lakini wenyewe *TIB* wanaweza wakaunda Idara ya kutoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo ili mradi Serikali iweke *guarantee* yaani Serikali iweke *guarantee* kwamba wakipata hasara basi Hazina ilipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunakubali, kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Christopher Chiza, kuwa hii ni hoja nzuri, lakini inahitaji mchakato, inahitaji tuitazame kwa makini kwamba tunazo benki ambazo tayari zinafanya kazi za *Microfinance.* Tumeielekeza *NMB* kwa makusudi ijiimarishe kwanza kabla haijaanza kutoa mikopo. Serikali tunaichukua hoja na tunaangalia jinsi gani *NMB* inaweza kurekebishwa ili ishughulikie mikopo kwa wakulima wadogo wadogo yaani *microfinances,* inaweza ikafanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimjibu Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, ambaye alitoa wazo zuri sana kwamba mchakato wa kuimarisha *TIB* umechukua muda mrefu ili kufikisha mtaji wa *fifty billion*. Napenda kumshukuru sana kwa wazo alilolitoa kwamba kwa nini tusiombe Benki Kuu ikachangia mtaji wa shilingi bilioni 10, tukayaomba Mashirika yetu ya Hifadhi ya Jamii na yenyewe yakatoa shilingi bilioni tano tano tukapata bilioni 20, kwa hiyo zikapatikana bilioni 30. Kwa hiyo, *TIB* ikapata mtaji mkubwa mapema ili iweze kufanya kazi zile ambazo zimekusudiwa.

Nasema namshukuru kwa wazo hilo ambalo alikwishalitoa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi. Tunalichukua, tutajaribu kuzungumza na Benki Kuu, tutazungumza na vyombo vyote vya fedha na kwa bahati nzuri vyote ni vya Serikali. Kwa sababu ni mtaji siyo kwamba vinatoa mkopo. Nadhani tunaweza tukafikia muafaka na kuyashawishi Mashirika hayo kuwekeza mtaji katika *TIB*. Bunge lako Tukufu litaarifiwa hatua zitakazokuwa zimefikiwa katika kuboresha mtaji wa *TIB.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka pia nipendekeze kwamba sasa hivi Serikali imeruhusu kuundwa Benki za Jamii, *Community Development Bank*, wanaweza kuunda Benki za Kiwilaya, wanaweza kuunda Benki kwenye Mkoa. Kwenye Wilaya kwa mtaji wa shilingi milioni 500 mnaweza kuanzisha Benki ya Jamii, kwenye Mkoa kama shilingi bilioni 2 mnaweza kuanzisha Benki ya Jamii. Sasa tukiweza kuunda Benki ya Jamii kwenye Mkoa na jukumu mojawapo likawa ni hili la kutoa *Microfinance*, mimi nafikiri mikopo ya wakulima wadogo wadogo inaweza ikapatikana kwa urahisi zaidi. Kule ambako Benki hizi zimeanzishwa Mbinga, Mufindi, Mwanga na mahali pengine kwa kweli wamepata mafanikio makubwa na wakulima wao wadogo wanapata mikopo ya kilimo na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kuanzisha Benki ya Wakulima ni zuri lakini linahitaji mchakato na maandalizi mazuri. Wakati mchakato huo unaendelea, tutaangalia kama *NMB,* Idara ya *Microfinance,* wataweza kusaidia kutoa fedha za mikopo kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa niaba ya Wizara ya Fedha na kuahidi kwamba tutalifanyia kazi wazo hili kama Serikali kwa ujumla wake, lakini limekuja ghafla mno, na tungeelezwa mapema kwamba kinachokuja kuletwa Bungeni ni kuhusu kuundwa kwa Benki ya Kilimo tungekuwa tumejiandaa vizuri zaidi. Mimi na Waziri wangu tulikuwa tumejiandaa kujibu hoja za *TIB,* lakini sasa nimekuja kukuta kwamba hoja inahusu kuundwa Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunalikubali, tutalifanyia kazi na nataka kuwahakikishia kwamba tutakapokuja kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009, nadhani maombi hayo yatakuwa yamekwishashughulikiwa na tutaweza kuliambia Bunge kwamba tumefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nyingine. Awali nilikuwa nimetoa hoja hapa kwamba Bunge lako Tukufu lipokee hoja hii na kuijadili. Sasa nashukuru sana kwamba hoja imepokelewa na imejadiliwa na imeungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata wachangiaji 14. Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni hao wafuatao na ninaomba niwatambue: Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Christopher Chiza, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi wapo wanne, nao ni Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Clemence Lyamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kungekuwa na utaratibu wa kutambua mchango wa kunong’ona, kuna mmoja akaninong’oneza kwamba anaunga mkono hoja yangu na napenda nimtambue ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuishukuru sana Serikali kwa jinsi ilivyopokea hoja hii, na naamini kwamba kwa kweli ni hoja ya nchi nzima. Kwa sababu watu wengi tunaowazungumzia hapa ni wakulima wanaoishi vijijini. Kwa hiyo, hoja hii inagusa karibu kila familia na wengi tuliomo humu ndani ni watoto wa wakulima tumehamia tu mjini. Kwa hiyo, bado kuna haja sana kuangalia maendeleo ya vijijini.

Nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwamba hoja ilikuwa ya *TIB*.

Mimi nilichotafuta ni mahali pa kuanzia hoja yangu na ni hapo. Kwa sababu jukumu moja la *TIB* ni kutoa mikopo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya shughuli za uzalishaji na maendeleo. Sasa nilipochambua kitabu kile nikakuta kuna mikopo imetolewa kwenye kilimo, nikasema ni hapa hapa sijaona taarifa nyingine ambayo imezungumzia kilimo katika taarifa hizo zinazohusu mabenki, hakuna. Kwa hiyo, mimi nawashukuru kwamba wameiona hiyo. Nadhani labda ni mawasiliano tu, hata mimi niliarifiwa tu Jumamosi kwamba hoja yangu itakuwa kwenye Bunge leo na nikajitahidi kuweka maudhui ambayo yatawafanya wenzangu wawe pamoja na mimi, na waelewe nini ninachotaka kukizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichopata hapa ni kwamba kwa kweli wote tumekubaliana kwamba kuna haja ya kuanzisha utaratibu mahususi wa ukopeshaji kwa ajili ya wakulima wadogo. Utaratibu mahususi wa kuwakopeshaji wakulima wadogo. Kwa sababu hao wakulima wakubwa nimewaona katika *TIB*, sikuona mkulima mdogo hata mmoja. Kwa hiyo, uanzishwaji wa Benki Maalumu kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wadogo, hiyo ndiyo hoja hasa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata michango ya maandishi, nitaiweka ili niwakabidhi ambao baadaye wataendeleza suala hili. Lakini nilichopata hapa ni kwamba utaratibu au mawazo haya ya kuweka utaratibu mahususi yamekubaliwa na wote. Hilo ni moja. La pili, kuanzishwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wadogo limekubaliwa. Mengine yaliyojitokeza ni kwamba kuna njia mbalimbali za kutumia hapa, inawezekana tukatumia *TIB* kwa kuipa Idara Maalumu kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wadogo, hiyo inawezekana. Tunaweza tukatumia utaratibu wa *NMB* wa kutenga sehemu kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kutahadharisha kwamba *TIB* hisa zake nyingi ni za Serikali yenyewe, hapo unaweza kucheza nayo kwa njia yoyote ile. *NMB* ina hisa za watu wengine, wanaweza kufika mahali wakasema hapana, hao watu wanasumbua mno mpaka uwafuatilie huko vijijini watatufanya tutafute utaratibu ambao hautaingiliana na hizi shughuli za siku hadi siku za mabenki ili ziweze kufanya kazi zao jinsi inavyotakiwa, kwa sababu wenye hisa wanaweza kukataa kwamba hii, hapana. Lakini kwenye *TIB* ndipo tulipoanzia nadhani tungeendelea hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana samahani Mheshimiwa Godfrey Zambi, nadhani wakati anaanza kuzungumza sikukumbuka kumwandika jina lake. Kwa hiyo, namtambua kwamba amechangia kwa kuzungumza na namshukuru sana kwa mchango wake. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho tunazungumzia ni Benki ya Kilimo na kuna wengine wameonyesha wasiwasi, lakini Kimataifa unapozungumza kilimo ni pamoja na kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na ufugaji wa nyuki. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mwinchoum Msomi kwamba katika hali hii ya kuanzisha

utaratibu wa kukopesha wakulima wadogo kwa kweli tungesema wajasirimali wadogo kwenye kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na shughuli zingine za nyuki na kadhalika wote hao wahusike.

Kwa hiyo, nadhani tutafute mahali ambapo wote hao watakubalika ili hata lile suala la kurasimisha rasilimali ambalo limezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge liunganishwe na hilo kwamba kama unajua mtu ana mali, lakini hana hati na wazee kijijini wamethibitisha kwamba hiyo mali ni ya kwake, basi asicheleweshwe mpaka msimu wa kilimo ukapita wakati mchakato unaendelea. Hiki ndicho kitu ambacho tunataka mahali hapo ataeleweka mkulima huyo kwamba hatua ya kupata hati inachukua muda mrefu, lakini kilimo kinakwenda pamoja na msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya kilimo linaangalia vitu vingi. Kwa hiyo, tunavyozungumza mikopo ya kilimo, kwa kweli ni pamoja na yale *bulldozers* aliyozungumzia Mheshimiwa Raynald Mrope kusafisha mashamba, kununua mifugo mipya na zana zingine za kufanyia kazi hiyo. Ninachotaka kusema ni kwamba suala hili siyo la kuchelewesha, nimelileta leo na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, amesema litashughulikiwa tuseme kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha ili liingie katika mwaka wa fedha 2008/2009, namshukuru sana. Sasa tuichukue hiyo kama ndiyo *timeframe* yetu.

Kwa hiyo, lifanyiwe kazi na kuna mawazo yametolewa kwamba katika kulifanyia kazi hilo turuhusu Serikali itumie utaratibu wa kuunda jopo la wataalamu pamoja na wanasiasa kulizungumzia zaidi na hata kutafuta uzoefu wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu leo nashukuru kwamba suala hili limepokelewa na kwamba litafanyiwa kazi. Kwa hiyo,Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kuniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. RAYNALD MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(*Bunge lilipokea, kujadili na kuikubali hoja ya Mheshimiwa William H.Shellukindo)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa William Shellukindo, lakini wengi tumejifunza kwamba tunayo fursa katika Kanuni zetu za Bunge ambapo Mheshimiwa Mbunge anaweza akaleta hoja kama alivyofanya Mheshimiwa William Shellukindo kwa kuleta hoja yenye nia ya kujenga. Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo sina la zaidi, Shughuli za Bunge zilizopangwa Mezani hapa kwa asubuhi ya leo ni tatu.

Tulikuwa na maswali na yote yamejibwa, tulikuwa na Kauli za Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alikuja akatoa kauli ya Serikali na mwisho tulikuwa na hoja za Wabunge ambayo ni hoja kuhusiana na kujadili Taarifa ya Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* ambayo imetolewa na Mheshimiwa William Shellukindo na yenyewe tumeisikiliza na kuifikisha mwishoni. Kwa kuwa hakuna Shughuli nyingine iliyobaki kwa siku ya leo, nachukua fursa hii basi kuahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho Saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.57 Mchana Bunge Liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 13 Novemba, 2007 Saa 3.00 Asubuhi)*